

RAHA YA KIJORA

UKURASA 13




Cavani afunguka klabu kumgombea

UKURASA 22








# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

Jumapili Oktoba 11, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0580365

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


# BALAA JIPYA

• **Muhimbili** yabaini ongezeko watoto wanaozaliwa bila mfumo wa haja kubwa, kila wiki wagonjwa 10, chanzo chatajwa... *Endelea ukurasa 4*

## YALIYOMO


UKURASA WA 2
**CHADEMA YAHOJI ZINAKOTENGENEZWA FOMU ZA KUPIGA KURA UCHAGUZI MKUU**

UKURASA WA 2
**MAJALIWA ATAJA SABABU JPM KUCHAGULIWA TENA**


## Mgombea kitanzini Kamati ya Maadili

UKURASA 3



Freeman Mbowe IGP Simon Sirro

# IGP aagiza uchunguzi polisi aliyemwambia Mbowe hatashinda

UKURASA 2





Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

GET IT ON Google Play  Download on the App Store

**Fursa kwa Wagombea! 2020**

VOTE

Gazeti la Nipashe linawapongeza wateule wote waliopitishwa na vyama vyao kugombea ubunge katika majimbo mbalimbali nchini

Je ungependa kukishukuru chama chako ?

Je ungependa kutangaza sera zako kwa wapiga kura ?

Nipashe inatoa nafasi kutangaza sera zako kwa gharama nafuu

Nipashe MWANGA WA JAMII

Wasiliana nasi
Simu: 0686 101335,
Barua pepe: advertise@guardian.co.tz

VOTE

# IGP Sirro aagiza uchunguzi polisi aliyemwambia Mbowe hashindi

**Na Romana Mallya**

MKUU wa Jeshi la Polisi nchini (IGP), Simon Sirro, amesema timu kutoka Makao Makuu ya jeshi hilo iko mkoani Kilimanjaro kufanya uchunguzi wa video ya ofisa wa polisi anayedaiwa kumwambia Mgombea Ubunge wa Hai (CHADEMA), Freeman Mbowe, hatashinda katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu.

Video hiyo iliyosambaa kwa kasi kwenye mitandao ya kijamii katikati ya wiki hii, inamwonyesha ofisa huyo wa polisi akijibizana na Mbowe, ofisa huyo akisikika akisema 'utamshinda yule? huwezi kumshinda, unawadanganya wananchi kuwa utamshinda."

Katika majibizano hayo, ofisa huyo aliyekuwa na mavazi ya Jeshi la Polisi, pia alisikika akimwambia Mbowe kuwa anasababisha watu wanamfuata na kumtaka aingie kwenye gari.

"Mnafanya watu wanakuja, ingia kwenye gari tuondoke," alisikika ofisa huyo huku Mbowe akimjibu "sawa, msifukuzie watu wangu, watu wanifuate niwakimbie, hapana!"

Baada ya Mbowe kutoa kauli hiyo, ofisa huyo akasema: "Huwezi kumshinda hata ufanyeje, humshindi, ingia kwenye gari uondoke, yaani mawazo yako unawadanganya wananchi utamshinda, humshindi."

Akizungumza kuhusu video hiyo jana, IGP Sirro alikiri kuiona na kuweka wazi kwamba, tayari timu kutoka Makao Makuu ya Jeshi la Polisi imekwenda kulichunguza tukio hilo kwa kuwa kabla ya kufanya uchunguzi, hawapaswi kulaumu pande zote mbili.

"Nimeiona video hii na tunavyozungumza, timu yetu kutoka Makao Makuu tayari imekwenda kuchunguza hilo tukio kuona kuna nini. Suala la majibu kwamba utashinda au utashindwa, hiyo siyo kazi ya polisi, ni kazi ya tume (Tume ya Taifa ya Uchaguzi NEC).

"Tunachunguza, tukiona kuna jambo la ukweli kutokana na ile video tuliyoiona, basi tutachukua hatua dhidi ya huyo ofisa. Jeshi lina kanuni zake na tuna kanuni za kudumu, wanasema 'Police General Order', ile inatuongoza sana, lakini pia tuna sheria za Jeshi la Polisi na za maofisa wasaidizi pia na maelekezo.

"Kimsingi kamanda anapokwenda tofauti, polisi ofisa anapokwenda tofauti, ipo miongozo na maelekezo yanayotawala utendaji wetu, basi tunamwajibisha kwa mujibu wa taratibu zetu, kwa hiyo wanaelewa," alisisitiza.




Mjumbe wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM, Kassim Majaliwa, akimkabidhi Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2020-2025, Mgombea Ubunge wa CCM katika jimbo la Mkinga, Dastan Kitandula (kushoto) na Mgombea Udiwani Kata ya Daluni, Mwanakombo Gobeto, wakati wa mkutano wa kampeni wilayani Mkinga, Mkoa wa Tanga, jana. **PICHA: OWM**

# Majaliwa: Tumchague JPM, tumemjaribu na ameweza

**Na Mwandishi Wetu,** MKINGA

MJUMBE wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa ya Chama cha Mapinduzi (CCM), Kassim Majaliwa, amesema ni muhimu Watanzania kutumia busara kwa kumchagua tena Dk. John Magufuli, ili aendelee kuliletea taifa maendeleo.

Alitoa kauli hiyo jana alipozungumza na wananchi wa Kata ya Daluni wilayani Mkinga mkoani Tanga katika mkutano wa kampeni za kumwombea kura Dk. Magufuli, mgombea ubunge wa Mkinga, Dastan Kitandula na wagombea udiwani kwa tiketi ya CCM.

"Rais John Pombe Magufuli ndiye mgombea mwenye sifa thabiti za kuliongoza taifa hili na katika kipindi cha miaka mitano ya uongozi wake, amewatumikia Watanzania kwa uaminifu mkubwa na mnajua ni kwa namna gani ambavyo ametuletea maendeleo watu wote bila kujali vyama, makabila na uwezo wetu, alisema.

Majaliwa alisema Dk. Magufuli amefanya maboresho makubwa katika utoaji wa huduma mbalimbali za kijamii ikiwa ni pamoja utoaji elimumsingi bila ada na kuwawezesha watoto kusoma bure na bila ya ubaguzi wowote.

Alisema Dk. Magufuli pia ameboresha huduma za afya na kuwawezesha wananchi kutibiwa karibu na makazi yao, akisisitiza: "Maendeleo hayana chama, tukamchague Dk. Magufuli, ni mchapakazi."

Alisema kupitia Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2020-2025, serikali itaendelea kuboresha zaidi utoaji wa huduma za kijamii, hivyo akawaomba Watanzania wahakikishe Oktoba 28 wanajitokeza kwa wingi kwenda kuwachagua wagombea wa CCM katika ngazi ya urais, ubunge na udiwani.

Majaliwa pia alisema serikali imekamilisha taratibu za kuwagawia wananchi shamba la Mwele lililoko wilayani Mkinga, ili walitumie kwa ajili ya shughuli za kilimo, baada ya shamba hilo kuachwa kwa muda mrefu bila ya kuendelezwa.

Alisema mashamba matano ya mkonge yanayomilikiwa na Bodi ya Mkonge pamoja na mashamba mengine ambayo hayajaendelezwa, serikali imeagiza yagawiwe kwa wananchi walime mkonge na kujikwamua kiuchumi.

## CHADEMA yahoji zinakotengenezwa fomu za kupiga kura uchaguzi mkuu

**Na Romana Mallya**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kimeitaka Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), ijitokeze hadharani na kutaja kampuni iliyoshinda zabuni ya kuchapisha karatasi za kupiga kura katika uchaguzi mkuu wa Oktoba 28, mwaka huu.

Hata hivyo, tume hiyo kupitia kwa Mkurugenzi wake, Dk. Wilson Charles, imesema ilishatangaza zabuni hiyo kwenye mfumo wa ununuzi wa umma kwa njia ya kieletroniki, hivyo kuwataka CHADEMA waangalie huko kuijua kampuni iliyoshinda.

Jana, Katibu Mkuu wa CHADEMA, John Mnyika, aliwaambia waandishi wa habari jijini Dar es Salaam kuwa Juni 30, mwaka huu, Mwenyekiti wa NEC, Jaji mstaafu Semistocles Kaijage, alisema tume itasema kampuni iliyoshinda zabuni hiyo iliyotangazwa Machi 9, mwaka huu.

"Machi 9, NEC ilitangaza kwenye vyombo vya habari zabuni ya kuitisha kampuni za kuchapisha karatasi za kupigia kura. Taratibu za ununuzi zinataka baada ya kuitisha, ilitakiwa kutoa taarifa kuhusu kampuni gani zilishindanishwa na iliyoteuliwa kuchapisha karatasi hizo," Mnyika alisema.

Kiongozi huyo wa chama alisema tangu kipindi hicho, ni karibu miezi minne tume haijatangaza kampuni ilishinda zabuni hiyo.

"Hata kamati ya zabuni ya ununuzi inayohusisha vyama vya siasa katika kikao chake cha tarehe nane mwezi huu (Oktoba 8, 2020), hakijaelezwa na NEC jina la kampuni iliyopewa kazi hii," alisema.

Mnyika alidai kuwa, kupitia vyanzo vyao, wamebaini ipo kampuni ya Tanzania iliyopewa zabuni hiyo wakati awali ilitajwa kampuni ya Afrika Kusini.

"NEC ieleze ni kampuni gani iliyopewa kazi ya kuchapisha karatasi za kupigia kura kati ya hizi mbili; ya Tanzania au Afrika Kusini. Iwapo imebadili mchapishaji, ieleze ni mchakato gani wa ununuzi ulipitiwa kwenye kuteua kampuni ya kuchapisha karatasi hizi," Mnyika alisema.

Katibu Mkuu huyo alisema endapo ikithibitisha kampuni iliyoteuliwa ni ya Tanzania, NEC itapaswa kuwahakikisha Watanzania usalama wa karatasi hizo.

"Mchapisha karatasi za kura asipokuwa mtu salama mwenye kuaminika na taasisi huru, upo uwezekano wa kuchapishwa karatasi za ziada. Ili uchaguzi usiwe wa hujuma, tume ijitokeze hadharani ieleze ni kampuni gani iliyopewa zabuni," alisisitiza.

Alipotafutwa na Nipashe jana kuzungumzia hoja hizo za CHADEMA, Dk. Charles, alisema NEC haijatangaza hadharani kampuni iliyoshinda kwa sababu zabuni ilitangazwa kwenye mfumo na kampuni zilizoomba, nyingi ni za nje.

"Wasitake kuleta taharuki za uongo, waangalie kwenye mfumo tulitangaza, wanajua na zilizoshinda mfumo unaonyesha," alisema mkurugenzi huyo na kusisitiza kampuni zilizoomba zilifuata utaratibu.

"Waambie tulitangaza kwenye mfumo na zilikuwa ni zabuni za kimataifa, walioshinda wanajulikana, wapo kwenye mfumo, hayo wanasema uongo, muda wa kampeni utaisha mambo yote ya uongo uongo yataisha, watabaki wametulia," alisema.

HABARI KITAIFA

# Akumbusha Watanzania kumuenzi Baba wa Taifa

**Na Vincent Mpepo,** OUT

OFISA Mhifadhi Mwandamizi, ametaka Watanzania kuendeleza mazuri na mema aliyoyaasisi Baba wa Taifa, Hayari Mwalimu Julius Nyerere, ili nchi iendelee kuwa na umoja, amani na utulivu licha ya matatizo mbalimbali inayopitia.

Neema Mbwana alitoa rai hiyo jana jijini Dar es Salaam alipongumzia maandalizi ya uzinduzi wa nyumba ya kihistoria ambayo aliishi Baba wa Taifa wakati wa harakati za kupigania uhuru wa nchi.

Alisema Baba wa Taifa alikuwa kiongozi shupavu na mwenye kujali maslahi ya umma ndiyo maana aliipigania nchi kwa hali na mali ili kuhakikisa inakuwa huru.

Mbwana alisema ukarabati wa nyumba hiyo ya kihistoria umefanywa na Shirika la Hifadhi ya Taifa (TANAPA), akibainisha kuwa nyumba hiyo itawezesha kuwapo kwa uhifadhi wa kihistoria.

"Nyumba hii ipo katika mtaa ambao una nyumba za viongozi waanzilishi wa taifa letu wakiwamo Kandoro, Kaluta, Lucy Lameck na Rupia," alisema.

Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Uhifadhi (Idara ya Mawasiliano), Paschal Shelutete, alisema TANAPA imejipanga vyema kutoa elimu shuleni kuhusu masuala ya uhifadhi wa malikale na umuhimu wa uhifadhi wa Nyumba Kumbukizi ya Mwalimu Nyerere katika Jiji la Dar es Salaam.

Alisema nyumba hiyo imefanyiwa ukarabati mkubwa uliopanza Machi 2019 chini ya TANAPA kupitia Mkandarasi (SUMA JKT) na mtaalamu mshauri kutoka Wakala wa Majengo (TBA).

Alisema kazi za ukarabati wa jengo zimefanyika kama ilivyokuwa kwenye makubaliano yaliyoafikiwa na pande zote tatu.

"Usimamizi wa kitaalamu ulifanywa na Idara ya Malikale ili kuhakikisha sheria zote za uhifadhi zinazingatiwa", alisema Shelutete.

Watanzania wataendelea kumkumbuka Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Nyerere ambaye alifariki dunia Oktoba 14, 1999 ikiwa ni takribani miaka 21 sasa.

# Mgombea kitanzini Kamati ya Maadili

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MGOMBEA Ubunge wa Shinyanga Mjini (CHADEMA), Salome Makamba, ameitwa kwenye Kamati ya Maadili ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), akidaiwa kukiuka masharti ya kuendesha kampeni.

Tuhuma zilizotolewa dhidi yake ni kutumia vijana wa chama chake kuchana mabango ya mgombea mwenzake katika jimbo hilo, Patrobas Katambi (CCM) na kumzushia mpinzani wake huyo kuwa ana genge la majambazi.

Akizungumza na waandishi wa habari nje ya Ofisi za Mkurugenzi wa Manispaa ya Shinyanga, Geoffrey Mwangulumbi, ambaye ndiye msimamizi wa uchaguzi katika jimbo hilo, Makamba alidai kutohusika na tuhuma hizo zinazoelekezwa dhidi yake.

"Nimeitwa kwenye Kamati ya Maadili kwa mara ya pili sasa nikilalamikiwa kuchana mabango ya mgombea wa CCM Jimbo la Shinyanga Mjini, Patrobas Katambi, tuhuma ambazo siyo za kweli, ukiangalia mji mzima mimi ndiyo sina, mabango yangu yote yamechanwa.

"Kwa upande wa kutoa lugha chafu za kukashfu jinsi ya kike, ushahidi huo ninao na nitauleta, ila ninapenda kutoa tu wito kwa wagombea wenzangu hapa Shinyanga Mjini, tushindane kwa kunadi sera na hoja na siyo kutumia lugha chafu za matusi," alisema.

Msimamizi wa Uchaguzi Jimbo la Shinyanga Mjini, Mwangulumbi, alikiri mgombea huyo kuitwa kwenye kamati hiyo ili kujibu tuhuma zinazomkabili dhidi ya mgombea mwenzake wa CCM.

Mwangulumbi alisema kwamba, baada ya kusikiliza utetezi wake, kamati ilitarajiwa kutoa uamuzi wake ndani ya saa 48 kwa mujibu wa sheria.



Mgombea Ubunge Jimbo la Shinyanga mjini (CHADEMA), Salome Makamba, akielezea namna alivyoitwa kwenye kamati ya maadili ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), kwa madai ya kukiuka sheria za uchaguzi. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Bashiru atoa mbinu kwa vijana kukabili ubeberu

**Na Gwamaka Alipipi**

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Bashiru Ally, amewataka vijana nchini kujua historia ili kuepukana na vikwazo, dhambi za ubeberu na dhana ya ubaguzi wa rangi.

Amesema vijana wakijifunza na kufahamu historia ya nchi yao vizuri, watakuwa na uwezo wa kupambana na ubeberu pamoja na ukoloni.

Alitoa rai hiyo jana wilayani Kibaha mkoani Pwani, alipotembelea Chuo cha Uongozi cha Mwalimu Julius Nyerere, ambacho kitakuwa mahususi kujifunza masuala ya uongozi, itikadi, mapambano dhidi ya ubeberu na ubaguzi wa rangi.



"Ni chuo ambacho kimejengwa kwa ushirikiano wa vyama sita vya ukombozi barani Afrika; CCM, ANC, SWAPO, NPRA, ZANU-PF na FRELIMO, ikiwa ni sehemu ya kumbukizi ya mchango wa Mwalimu Julius Nyerere katika kupigania ukombozi wa nchi za Afrika.

"Hivyo, viongozi mbalimbali watajifunza masuala ya kiuongozi, na ni mradi uliojengwa kwa viwango vya kimataifa," alisema Dk. Bashiru.

Kiongozi huyo wa CCM, alisema chuo hicho hakijaitwa jina la Mwalimu Nyerere kwa bahati mbaya, bali kimepewa jina hilo kwa sababu alikuwa ni mwanasiasa, mwanafalsafa bora na mwanamapinduzi wa Bara la Afrika.

"Vyama vya ukombozi vilivyoshiriki katika ujenzi wa chuo hiki vitamuenzi Mwalimu Nyerere katika kupinga ubaguzi wa rangi na ukoloni. Hiki ni kituo cha mapambano ya kifikra na kiitikadi.

"Siasa ni msingi mkuu wa maendeleo, hata Azimio la Arusha, linabainisha kuwa ili tuelendelee, tunahitaji watu, ardhi, siasa safi na uongozi bora. Hivyo, huwezi kuongoza nchi kwa demokrasia na haki bila ya kuwa na viongozi walioandaliwa kwa itikadi na siasa," alifafanua.

Kuhusu CRJE iliyojenga chuo hicho, Dk. Bashiru alisema ni miongozi mwa kampuni zilizopewa heshima kubwa nchini kwa kujenga miradi mikubwa minne, ikiwamo Daraja la Nyerere (Kigamboni) na Reli ya TAZARA.

Balozi wa China nchini, Wang Ke, alisema ushirikiano kati ya Tanzania na China ni wa miaka mingi na utaendelea kudumu, akisisitiza kuwa Tanzania ni sehemu yenye amani na mataifa mengine yanapaswa kuja kujifunza.

# Kuzaliwa bila mfumo haja kubwa: Ugonjwa unaotikisa madaktari bingwa Muhimbili

- Matibabu yake yanachukua miaka miwili
- Mgonjwa lazima apasuliwe awamu tatu

**Na Mary Geofrey**

WAKATI nchi ikiwa katika harakati za kuboresha matibabu ya kibingwa, Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) imebainisha ongezeko la watoto kuzaliwa pasi na mfumo wa kutolea haja kubwa.

Takwimu za hospitali hiyo inayotoa matibabu ya ugonjwa huo, zinabainisha inapokea watoto saba hadi 10 kila wiki kutoka maeneo mbalimbali nchini wakihitaji matibabu hayo.

Vilevile, takwimu za MNH pia zinaonyesha watoto watatu huzaliwa na tatizo hilo kila wiki katika hospitali hiyo kubwa zaidi nchini.

Daktari Bingwa wa Upasuji wa Watoto wa MNH, Dk. Zaituni Bohari (pichani), katika mahojiano yake maalum na Nipashe jijini Dar es Salaam, anabainisha ukubwa wa tatizo hilo akisema kwa wiki wanafanya upasuji kwa watoto wawili hadi watatu wenye shida hiyo.

Mtaalamu huyo wa magonjwa ya watoto anasema mtoto kuzaliwa pasipo kuwa na njia ya haja kubwa ni tatizo lililogawanyika katika maeneo mawili na kuna kwamba tofauti kubwa ya matibabu yake kati ya watoto wa kike na kiume.

Anasema wapo watoto wanaozaliwa wakiwa na ishara au alama ya kuwapo kwa shimo la kupitishia haja kubwa na inakuwa inaonyesha kuwa kuna utumbo mkubwa wa kupitishia haja kwenye eneo hilo.

Hali kadhalika, Dk. Bohari anasema kuna watoto wengine wanazaliwa wakiwa hawana ishara wala kuonyesha kama kunatakiwa kuwa na tundu la kutolea haja kubwa.

Anasema kuwa, kwa wagonjwa wasio na ishara ya shimo la kutolea haja kubwa, upasuaji wake unakuwa mgumu kufanyika kutafuta sehemu ya kutoboa ili kupata utumbo unaopitisha haja kubwa.

"Mgonjwa ambaye hana kabisa shimo ni shida kumtibu kwa sababu anakosa misuli ya kuzuia haja hata baada ya kufanyiwa upasuaji," anabainisha Dk. Bohari.

Anafafanua kwamba, kutokana na kukosa misuli, tundu hilo la kutolea haja kubwa kuna uwezekano mkubwa lisifanye kazi vizuri na kusababisha haja kubwa kutoka yenyewe.

Anasema mbinu wanayoitumika kumaliza tatizo hilo, ni kuhahakikisha mgonjwa anapatiwa mazoezi maalum ya kukaza misuli ya kuzuia choo baada ya kukamilisha upasuaji.

Kuhusu wagonjwa wenye ishara ya tundu la kutolea haja kubwa, Dk. Bohari anasema inakuwa rahisi kufanya upasuaji na kuupata utumbo mkubwa unaopitisha haja kubwa.

"Mara baada ya upasuaji, mgonjwa kama huyu anakuwa sawa na kuendelea kupata choo kama kawaida bila shida yoyote ile," anasema.

### SHIDA ZA KIJINSIA

Dk. Bohari anasema kwa watoto wa kike, tatizo hilo ni hatari zaidi kwa sababu siku za baadaye, hawaruhusiwi kujifungua kwa njia ya kawaida.



Dk. Zaituni Bohari. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

Anafafanua kuwa wakati wa kujifungua, hawaruhusu mwanamke aliyewahi kufanyiwa upasuaji huo, kujifungua kwa njia ya kawaida, kwa kuwa kunakuwa na uwezekano mkubwa wa kufumua shimo walilolitengeneza kwa ajili ya kupitisha haja kubwa.

Anasema kuwa, tundu hilo likishafumuka, huwa linaungana na njia ya haja ndogo kwa wanawake.

"Tukiwa tunawafanyia upasuaji watoto wa kike, tunawashauri kabisa wazazi wasiruhusu baadaye akajifungua kawaida. Tunawahimiza kutafuta daftari awaandikie kabisa iwe kumbukumbu kuwa wakifika umri wa kubeba ujauzito, wasiruhusu kujifungua kwa njia ya kawaida," anaonya.

Daktari huyo anaendelea kufafanua kuwa, watoto wa kike wasio na mfumo wa kutolea haja kubwa, kinyesi hushuhudiwa kikitoka kupitia njia ya haja ndogo na hata kitaalamu wanaweza kutoboa tundu kwa ajili ya haja kubwa likapita sehemu ya haja ndogo.

"Hawa watoto wa kike kuna ahueni kiasi, walau unaweza kukuta choo kinatoka kidogo kidogo katika njia nilizotaja na ndiyo sababu tunakataza wasizae kawaida. Watoto wa kiume hawana njia mbadala zaidi ya kutobolewa ubavuni ambako patatumika kupitisha choo kikubwa kwa muda," anasema.

Dk. Bohari anasema mtoto wa kiume ni rahisi kufanya upasuaji wa kumtengenezea njia ya haja kubwa kwa sababu hana njia mbadala ya kutolea haja.

Anasema upasuaji wake unatumia saa nne, lakini kwa mtoto wa kike ni mgumu kwa sababu maumbo yake ya haja kubwa na haja ndogo yapo karibu, hivyo unahitajika utaalamu wa hali ya juu.

### KIINI CHA TATIZO

Dk. Bohari anasema tatizo hilo halina chanzo maalum ingawa kitaalamu wanalihusisha na mfumo wa maisha tangu mtoto akiwa tumboni mwa mama.

Anasema tatizo hilo linasababishwa na maisha ya mama akiwa mjamzito kutokana na aina ya vyakula anavyokula na aina za dawa anazotumia ambazo kwa kiasi kikubwa zinaamua ajifungue mtoto mwenye afya au la.

"Ndiyo sababu wakati wa ujauzito tunasisitiza wajawazito kuhudhuria kliniki kwa ajili ya kupewa kinga za kuzuia magonjwa mbalimbali, kupata vitamini na maelekezo muhimu ya kuwasaidia kuzaa watoto imara na waliokamilika," anasema.

### MIAKA MIWILI

Dk. Bohari anasema matibabu ya ugonjwa huo hutumia miaka miwili hadi mtoto kupona na kuanza mwenyewe kutumia njia ya haja kubwa kutoa choo.

"Tujitahidi kula vizuri na kuhudhuria kliniki wakati wa ujauzito kwa sababu kumtunza mtoto ambaye hana sehemu ya haja kubwa ni shida kubwa sana," anaonya na kufafanua kuwa:

"Mtoto anazaliwa akiwa hapati choo. Kama hakitoki, maana yake kinabaki tumboni, kama kikibaki tumboni, tumbo linakuwa kubwa na kujaa, hivyo mtoto atashindwa kupumua vizuri na atapata homa kali."

Dk. Bohari anasema ni kutokana na uzito huo, huwa wanalazimika kufanya upasuaji wa dharura wa kumtoboa mtoto eneo la ubavuni ili kupitisha choo kwa muda.

### GHARAMA KUBWA

Mtaalamu huyo wa MNH anaweka wazi kuwa kuna shida mtoto kutumia njia ya ubavuni kutoa haja kubwa kwa sababu gharama zake ni kubwa.

Anasema kwa wenye uwezo mkubwa kifedha, wanatumia vifaa maalum vya kutolea uchafu ambavyo gharama yake kwa kimoja ni Sh. 3,500 hadi 7,000.

Dk. Bohari anasema mtoto anaweza kutumia eneo alilotobolewa kupitisha haja kwa kipindi cha hadi mwaka mmoja, hivyo mzazi atalazimika kutumia kuwa ananunua kifaa hicho kwa muda wote huo.

"Sasa, kwa wazazi wasio na uwezo mkubwa kiuchumi, wanaweza kutumia vitambaa kumkinga mtoto katika eneo lile na kuvibadilisha mara kwa mara.

"Jambo hili limekuwa linawaathiri wazazi kisaikolojia, wakiamini kuwa tatizo linaweza lisitibike kabisa kutokana na mateso wanayoyapata wakati wa kuuguza.

"Wakati mwingine mama anaweza kurukwa na akili, wengine kususa watoto wao kutokana na matatizo wanayoyapata katika kipindi hicho," Dk. Bohari anaanika ushuhuda wake.

Anasema kwa kuzingatia hali hiyo, anakumbusha wazazi kuzingatia taratibu sahihi za lishe na huduma kwa mjamzito ili kujifungua watoto wenye afya njema.

### UPASUAJI UNAVYOFANYIKA

Dk. Bohari anasema mara baada ya kumfanyia upasuaji huku akiwa na tundu la muda ubavuni kwa ajili ya kutolea haja kubwa, wanaendelea na kazi ya kumtengenezea mtoto njia kwa ajili ya kupitisha haja kubwa.

Anasema baada ya upasuaji, mtoto hupelekwa kliniki kwa ajili ya kutanuliwa njia ya haja kubwa kwa kutumia vyuma maalum vinavyoingizwa kwenye njia ya haja kubwa iliyotengenezwa.

"Kwa hiyo, suala hili linakuwa linawatesa kinamama kisaikolojia, lakini kwa sababu ni matibabu, tunalazimika kufanya na wengine huwa tunawafundisha kufanya wenyewe nyumbani ili njia isije ikaziba," anasema.

Dk. Bohari anasisitiza kuwa ni lazima kufanya mazoezi ya kutanua njia kwa sababu njia ikiziba, wanalazimika kufanya upya upasuaji ili kuitengeneza.

Anasema kuwa, baada ya upasuaji huo, wanafanya upasuaji mwingine wa kuziba tundu la kwanza walilolitengeneza ubavuni kwa ajili ya kupitisha haja kubwa.

Dk. Bohari anasema upasuaji wa awali wanafanya kama wa dharura na upasuaji wa pili mkubwa hujafanya baada ya mtoto kukua kidogo ili kupata uzito wa kustahimili.

"Tunaangalia na hali ya mtoto ndipo tumfanyie upasuaji, wengine tunachukua hadi mwaka kumsubiri apate nguvu ili ahimili kufanyiwa upasuaji huo mkubwa," anasema.

Anabainisha kuwa upasuaji wa tatu hufanya baada ya wiki sita baada ya upasaji mkubwa kufanyika, lengo likiwa kuhakikisha afya ya mtoto haiteterekі.

Anasema kwa ujumla mtoto hutumia hadi miaka miwili kufanyiwa matibabu hadi kupona na kuwa na uwezo wa kujisaidia kwa njia ya kawaida mwenyewe.

### NEEMA YA UTANDAWAZI

Dk. Bohari anasema anaamini ongezeko la wagonjwa wa aina hiyo kufikishwa hospitalini huko linatokana na maendeleo ya teknolojia na utandawazi.

Anasema watoto kama hao walikuwapo na walikuwa wakitengwa au kuuawa na ndiyo sababu iliwafanya wazazi wengi kushindwa kujitokeza kwa ajili ya matibabu ya watoto wao.

"Watoto kama hawa walikuwapo tangu zamani, lakini walikuwa wakifichwa kwa sababu za imani ya kishirikina, wazazi wakihofia kuuliwa au kutengwa na jamii," Dk. Bohari anafafanua.

RIPOTI MAALUM

# Wasiojulikana watafuna mamilioni ya Muhimbili

Na Mary Geofrey

***SAFU ya kwanza ya simulizi ya madhila haya Jumapili iliyopita, ilikuwa na uchambuzi unahusu kuwapo wagonjwa wanaokosa ndugu wasaidizi wanavyoteseka kwa upande mmoja na mwingine wanageuka mzigo wa kifedha na huduma kwa Taasisi ya Tiba ya Mifupa na Mishipa ya Fahamu Muhimbili (MOI).***

***Leo ni awamu ya mwendelezo uliosheheni ufafanuzi rasmi wa chanzo cha mzigo na tatizo lilikojificha, ukianishwa na wadau wakuu mbalimbali wanaohusika moja kwa moja na madhila hayo. Endelea kupata udadisi wa Nipashe kuhusu udani huo.***



Dk. Grace Magembe

Hapana shaka kila tatizo lina kiini chake, hali kadhalika ufafanuzi wenye ukweli. Katika hilo linalowahusu wagonjwa wa MOI, ufuatiliaji wa Nipashe ulifika mezani kwa Mkurugenzi wa Tiba wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Grace Maghembe, anayeanza kwa kukiri ukweli wa kinacholalamika hospitalini huko.

Anasema, wakati kuna sehemu kubwa ya mzigo huo inahusiana moja kwa moja na hitaji la fedha, serikali imekuwa ikigharimia bajeti ya kundi hilo kwa kuzingatia uhalisia wa uwezo kiuchumi.

"Serikali inafanya kazi kulingana na mapato yake yaliyopo na anapotokea mgonjwa wa namna hiyo, hatuwezi kuacha kumpa huduma, lakini pia hatuwezi kumhudumia kila mwananchi," anasema.

Dk. Maghembe anasema namna wanavyowasiliana na matabibu ni kwamba, hospitali zimekuwa zikiwahudumia wagonjwa wao wa aina hiyo na baadaye kuwasilisha wizarani taarifa za gharama za huduma kwa kundi hilo serikalini kuiwajibisha kuzilipia.

Anasema hatua zinazochukuliwa na serikali katika kupambana na mzigo wa bajeti na usumbufu wa kiundeshaji kwa matibabu yanayofanana na hayo, dira ya kiutendaji iliyoko serikalini ni mkakati wa kitaifa wa kuhakikisha kila mwananchi anakuwa na bima ya afya, itakayokuwa mkombozi wake kimatibabu wakati wowote.

"Ndiyo maana tunahimiza kila mwananchi kuwa na bima ya afya, ili linapotokea tatizo, apatiwe matibabu na kuipunguzia serikali mzigo," anafafanua pasi na kueleza kwa kina namna wanavyokidhi ugharimiaji matibabu kwa matukio ya sasa.

Kwa mujibu wa Meneja Ustawi wa Jamii na Uhusiano wa MOI, Jumaa Almas, sehemu kubwa ya wagonjwa hao wanaobeba mazingira tata ya matibabu, ulezi na gharama ni waathirika wa ajali za barabarani.

**KAMANDA TRAFIKI AFAFANUA**

Safari ya Nipashe kupata undani wa hilo ilitua ofisini kwa Kamanda wa Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani, Fotunatus Muslim, anayelalamika hatua ya kwanza kuisababishia matatizo hospitali, ni pale wapitanjia wanapowaingia majeruhi wa ajali badala ya kipaumbele cha huduma.

> Wanashindwa kufahamu kama mgonjwa angekuwa na bima angeweza kupata matibabu kwa uhuru bila kuipa serikali mzigo mkubwa.

Hata hivyo, anasema hakuna uhakika kama wanaopata ajali wanakuwa na vitambulisho au la, akiendelea: "Ni wito wangu kwa wananchi pindi inapotokea ajali, watoe msaada kwa majeruhi wakiwa eneo la tukio na siyo kuwasachi na kuwaibia mali zao."

Kamanda Muslim anaeleza mandhari ya kiusalama hadi kutokea madhila hayo ni kwamba, ni pale polisi wa Usalama Barabarani wanapokuwa hawajafika katika eneo hilo kusaidia stahiki za huduma.

Pamoja na mazingira hayo, Kamanda Muslim anasema kwa sasa ajali sababishi zimepungua kwa kiasi kikubwa baada ya hatua za udhibiti kuendelea kuboreshwa barabarani.

"Takwimu za ajali barabarani kupungua sina hapa ila ni jambo ambalo lipo wazi kabisa, ajali zimepungua kwa kiasi kikubwa nchini, hakuna ajali zile kubwa na mbaya tulizokuwa tunasikia za kusababisha vifo na majeruhi," anasema.

Wito wake kwa waendeshaji wa vyombo vya moto ni kwamba wachukue hatua za tahadhari kwa ajili ya usalama barabarani, jambo ambalo lina mchango mkubwa kunusuru madhara ya maisha na mali za watumiaji wa barabara.

**NGO, WADAU**

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika Lisilo la Kiserikali la Sikika, Irene Kiria, katika hilo anamfafanulia mwandishi, akisimamia Sera ya Afya Duniani, inaelekeza kwamba suala la matibabu ya dharura kwa wagonjwa wote ni la lazima.

Anafafanua uhalisia ni kwamba, wagonjwa wa aina hiyo wameingia hawakutarajia kilichowakuta, hivyo suala la matibabu yao linaelekeza ulazima bila kujali vigezo vya kisera na kisheria kama vile milki ya bima ya afya, ikizingatiwa wapo wanaokuwa wameshapoteza kumbukumbu au uwezo sahihi wa kujitambua.

Ushauri wa Kiria ni kwamba serikali ihakikishe ina bajeti mahususi ya kuhudumia kundi hilo, akifafanua: "Jukumu la kwanza la hospitali na watoa huduma za afya ni kuponya na sera ya huduma za dharura ni kutibu kwanza, bila ya kufahamu kama ana bima ya afya au hana, lengo ni kuokoa maisha kwanza kisha mengine yafuate."

Baadhi ya wananchi waliozungumza na Nipashe kuhusu suala hilo, wanashauri elimu iendelee kutolewa kwa jamii kuhusu umuhimu wa kuwa bima ya afya.

Maoni ya mwanamama Jesca Mosses, mkazi wa Jiji la Dar es Salaam, ni kwamba bado anabaki na mshangao ni namna gani waathirika wa ajali hawatambuliki hospitalini, licha ya watu sasa kuwa na vitambulisho vingi.

Hata hivyo, Kamanda wa Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani, Muslim, ameeleza msingi wa tatizo uko katika umma kuwaibia wanaopatwa na ajali ikizingatiwa ndiyo wanaounda wagonjwa wengi wa matibabu yanayopatikana MOI.

Mosses anasema gharama za matibabu pia ni kubwa, hivyo husababisha ndugu wengine kuamua kukaa kimya ili kusubiri atibiwe na hospitali ndipo wajitokeze.

"Wanashindwa kufahamu kama mgonjwa angekuwa na bima angeweza kupata matibabu kwa uhuru bila kuipa serikali izigo mkubwa," anasema Mosses.

Jumanne Kidungwa, mkazi mwingine wa jiji hilo la kibiashara, anaishauri serikali kutoa ruzuku kwa wananchi kukata bima ya afya kwa ajili ya kuhakikisha kila Mtanzania anapata bima yake, akiamini kwa kufanya hivyo kutaipunguzia serikali mzigo huo wa matibabu.

Anasema wananchi wanashindwa kumudu gharama za kuwa na bima ya afya kwa sababu ziko juu, hivyo licha ya juhudi za kuhamasisha kuwa nazo, serikali ichangie gharama kwa wananchi ili kila Mtanzania awe nayo.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kampeni ya nyumba ni choo itumike vita dhidi ya malaria

**KWA** miaka mingi nchini, kipindupindu kimekuwa kikiibuka mara kwa mara na kusababisha maafa ikiwamo vifo kwa wananchi, jambo ambalo limekuwa aibu kwa taifa kutokana na ukweli kwamba ni ugonjwa unaozuilika.

Ugonjwa huo ambao hutokana na watukuka uchafu ama kwa kujitambua au kutojitambua, ulikuwa ukigharimu maisha ya watu hasa vijana na watu wa makamo ambao ni nguvukazi ya taifa.

Wataalamu wa afya wamekuwa wakieleza bayana kwamba chanzo cha ugonjwa huo ni watu kula kinyesi kibichi kwa njia ya vyakula, matunda na vinywaji sambamba na matumizi mabaya ya vyoo au kukosekana kwa miundombinu hiyo.

Kutokana na kukosekana kwa vyoo, mathalan, watu wamekuwa wakijisaidia porini hatua ambayo imekuwa ikisababisha uchafu kusambaa hadi kwenye mito ambayo watu huteka maji kwa ajili ya matumizi mbalimbali. Maji hayo, baadhi ya kaya zimekuwa zikiyatumia kwa kunywa bila kuyachemsha na matokeo yake kuibuka kwa kipindupindu.

Jijini Dar es Salaam, kwa mfano, maeneo kama Buguruni, Mburahati, Tandale, Temeke, vingunguti na Ilala yalifikia hatua ya kuitwa makao makuu ya kipindupindu kutokana na kila mwaka kukumbwa na ugonjwa huo licha ya elimu iliyokuwa ikitolewa kila mwaka.

Hata hivyo serikali ilianzisha kampeni mahsusi ya kitaifa ya usafi wa mazingira miaka michache iliyopita iliyojulikana kama 'Usichukulie Poa Nyumba ni Choo' ambayo imeonyesha mafanikio makubwa kwa kupunguza magonjwa ya mlipuko, kipindupindu kikiwamo.

Kupitia kampeni hiyo, kwa mujibu wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, kaya nyingi zimeelimika kwa kunawa mikono pamoja na kujenga vyoo bora na imara. Kupitia kampeni hiyo, hivi sasa ni asilimia mbili tu ya kaya hazina vyoo kulinganisha na asilimia 6.1 iliyokuwapo mwaka 2015/16.

Kupungua kwa kiwango hicho cha nyumba zisizo na vyoo, si miujiza bali ni elimu, utashi na jitihada za makusudi zilizochukuliwa kuhakikisha azma hiyo inafanikiwa ili kuokoa maelfu ya Watanzania waliokuwa wakiangamia kutokana na magonjwa yanayoweza kuzuilika.

Kupungua kwa maradhi hayo ni hatua kubwa ya kujivunia kwani Tanzania imeandika rekodi katika Afrika kuwa moja ya nchi zilizopiga hatua katika mapambano dhidi ya kipindupindu na maradhi mengine.


Jitihada hizo, zinapaswa kuelekezwa katika mapambano dhidi ya magonjwa mengine ya kuambukiza kama malaria na kifua kikuu na yasiyo ya kuambukiza yakiwamo kisukari, maradhi ya moyo, mabusha na matende.

Malaria, kwa mfano, ni ugonjwa ambao unasababishwa na mbu kutokana na kuzaliana katika maji yaliyotuama kwenye mashimo, vifuu vya nazi, matairi mabovu na mashimo yenye maji. Hatua pekee ya kuanza kupambana na ugonjwa huo ni kufukia na kuteketeza mazalia ya mbu katika maeneo ya shughuli za uzalishaji na makazi.

Ni imani kwamba kampeni hii ikianzia katika ngazi za mitaa, kutakuwa na mafanikio makubwa katika kupambana na malaria na hatimaye kupunguza madhara yatokanayo na ugonjwa huo.

Matokeo yake vifo vinavyotokana na ugonjwa huo na kugharimu nguvu kazi ya taifa vitapungua kwa kiasi kikubwa. Kadhalika mamilioni ya fedha ambayo serikali imekuwa ikitumia katika matibabu na udhibiti, yataelekezwa katika shughuli za uzalishaji.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Dhana kwamba wanasiasa ni waongo ina ukweli gani?

**MWAKA** 1992 ndio ambao serikali ya Tanzania ilirejesha rasmi mfumo wa vyama vingi vya siasa, hatua ambayo ilisababisha baadhi ya Watanzania kuanzisha vyama hivyo kwa wingi.

Uchaguzi wa kwanza ndani ya mfumo, ulifanyika mwaka 1995 ambao baadhi ya vyama vilileta upinzani dhidi ya chama tawala- Chama Cha Mapinduzi (CCM) na kufanikiwa kupata wabunge na madiwani kutoka vyama hivyo.

Pamoja na hayo, kumekuwapo na wimbi la wanasiasa kuhama kutoka chama kimoja kwenda kingine, na wanafanya hivyo, kwa sababu ni haki yao ya kidemokrasia kujiunga na vyama wanavyovitaka.

Hata hivyo, baadhi yao wanapohama, wamekuwa wakitoa tuhuma nzito kuhusu kule wanakotoka na wengine kuapa kutorudi, lakini baadaye wanajikuta wamerudi huku wakiwa wameinamisha nyuso.

Katika kundi hilo, wako wale ambao husema kamwe hawawezi kuhama katika vyama vyao, lakini ghafla wanahama au kada wa chama fulani anasikika akisema kwamba mtu anayehama chama hicho hana akili.

Lakini cha kushangaza ni kwamba mwanasiasa huyo aliyewahi kutamka hayo, ndiye alikuwa wa kwanza kuhama chama chake na kujiunga na kingine hadi leo hajawahi kuhama.

Katika mwendelezo huo, kuna mwanasiasa kutoka Kanda ya Nyanda za Juu Kusini aliyewahi kukaririwa na vyombo vya habari akitangaza kuhama chama chake, wananchi wachome moto nyumba yake na mali zake.

Hiyo ilikuwa mwishoni mwa mwaka 2017, ikiwa ni muda mfupi baada ya kusambaa kwa taarifa za kutaka kukihama chama chake, lakini akadai hawezi kuhama kwa kuwa aliutafuta ubunge kwa gharama kubwa.

Katika msisitizo wake, alisema thamani ya ubunge haiwezi kushushwa kama vocha ya simu kwamba ikiisha unaweza kukwangua nyingine na kuweka msimamo wa kutohama.

Hata hivyo, mwanasiasa huyo tayari amesha-hama chama chake cha awali na kwenda kwingine, hali ambayo inaonyesha kuwa hakuweka akiba ya maneno katika kauli yake ya awali, kwa kubadili msimamo.

Mwanasiasa mwingine maarufu nchini, aliwahi kukaririwa na vyombo vya habari akisema, licha ya mambo anayofanyiwa na kunyang'anywa mashamba yake, hawezi kurudi chama fulani.

Huyo naye tayari amesharudi katika chama hicho alichokuwa anakikana, hali ambayo ni wazi inaweza kuwa inaipa nguvu dhana ambayo imejengeka vichwani mwa baadhi ya Watanzania kwamba, 'wanasiasa ni waongo'.

Kwa ujumla ni kwamba wako wanasiasa wengi tu ambao wamewahi kutoa kauli ambazo baadaye wanabadilika kimya kimya bila kutoa maelezo ya kina kwa mashabiki au wafuasi wa vyama vyao kuhusu uamuzi huo mpya.

Dhana hiyo ni ya kawaida kutoka vinywani mwa baadhi ya Watanzania, wakiwa na maana kwamba, wanasiasa siyo watu wa kuaminika, hivyo kauli zao zinafaa kupuuzwa.

Kwa dhana hii, ipo haja kwa wanasiasa wenye kuzitafakari zaidi kuona kama ina ukweli ndani yake ama wanasingiziwa tu na watu wasiowatakia mema, na kutengeneza mazingira ambayo yatarudisha imani kwa wapigakura.

Binafsi niseme kwamba yawezekana wako wanasiasa waongo kwa sababu wao si malaika bali ni binadamu kama walivyo wengine lakini kuwa na akiba ya maneno ni jambo la muhimu.

Wanasiasa kuwa na akiba ya maneno ni jambo la muhimu ili kuepuka kusutwa kwa kutoa ahadi ambazo hatima yake ni kuinamisha nyuso baada ya kukiuka kile ambacho huwa wamekiahidi awali.

jambo la msingi ni wanasiasa kuwa makini, kwa lengo la kutowachanganya wanachama ama wapigakura kutokana na kauli zisizokuwa na msimamo, ambazo baadhi yao wamekuwa wakizitoa.

Kabla ya kutoa kauli hadharani, ni vyema mhusika akajipa muda wa kutafari kwa kina ili kulinda jina lake katika jamii kuliko kutoa kauli ambazo baadaye anakuja kuzigeuka na kukosa uaminifu.

Suala la kuwa na akiba ya maneno ni la muhimu, ili mambo yanapobadilika, basi aweze kuwa na la kujitetea, kuliko ilivyo sasa, ambapo baadhi yao wanatoa kauli ambazo baadaye zinawasuta, wasitimize dhana hii ya 'wanasiasa ni waongo'.

SAFU

## FIKRA MBADALA



Nkwazi Mhango, Canada

# Elimu sawa ila bweni kwa vidudu hapana

MWISHONI mwa mwezi jana, taifa letu lilipata msiba mkubwa. Ni msiba uliohusisha watoto 10 huko Kyerwa, mkoani Kagera ambapo wahanga waliungua baada ya bweni la shule ya Kiislamu ya Byamungu kuwaka moto. Natoa salamu za rambirambi kwa wafiwa na taifa kwa ujumla. Pamoja na ukubwa wa msiba huu, kama jamii na taifa, kuna mambo tunayopaswa kujifunza kuepuka kurudia makosa kama watu wenye akili na uwezo wa kujifunza hata kufundisha. Hivyo, leo safu hii itaangalia masomo tunayoweza kupata kutokana na msiba huu. Pia tutaangalia baadhi ya upungufu uliofichuliwa na msiba huu katika maandalizi ya watoto wetu. Yafuatayo ni mambo muhimu kuzingatia:

Mosi, elimu ni ufunguo wa maisha. Hivyo, kila mzazi anajitahidi kuhakikisha anampa mtoto wake urithi borayaani elimu ili kumsaidia katika maisha yake ya baadaye. Hata hivyo, kuna angalizo hapa. Je ni wakati gani mzazi anapaswa kuanza kumpa mtoto elimu na katika mazingira gani? Jibu ni rahisi kuwa anapofikia umri wa kuelewa mafundisho. Je ni katika mazingira gani?

Pili, msiba tajwa hapo juu umeibua kitu kimoja ambacho wazazi wengi ama kwa kupofushwa na malengo yao mazuri ya kuwapa elimu na kuwaandalia maisha ya badaye watoto wao hushindwa kuona hatari ya baadhi ya namna elimu hii inavyotolewa. Mfano, wahanga walikuwa kwenye shule ya bweni ya msingi. Je ni busara kuacha watoto wa umri kati ya miaka sita hadi 13 kupelekwa kwenye shule ya bweni wakati ndiyo wakati muafaka wa kupata malezi ya wazazi wao nyumbani?

Tatu, tukizingatia umri wa wahanga, kwa mujibu wa gazeti moja la kila siku (si Nipashe) (Septemba 18, 2020), wahanga walikuwa wa umri kati ya miaka sita na 10, je, kwa mfumo wetu kuruhusu shule za msingi za bweni siyo upungufu ambao ukiachia mbali maafa ya moto ambayo yanaweza kumtokea yoyote yanaweza kusababisha maafa mengine kama vile udhalilishaji, ukosefu wa malezi ya wazazi hata kupoteza haki ya kufaidi utoto wao kwa watoto? Je, hapa mzazi anapaswa kuangalia umuhimu wa elimu au wa mtoto kulelewa naye kama sehemu ya haki na kanuni ya malezi ya kiafrika. Nitatoa mfano mzuri kuhusiana na malezi ya kiafrika tofauti na jamii nyingine. Sisi tangu tuishi hapa Kanada pamoja na utaratibu wa kupeleka watoto wachanga kwenye vituo vya kuangalia watoto (Day Cares) kwa sababu huku hakuna uwezekano wa kuwa na wasichana wa kazi hatujawahi kupeleka watoto wetu huko. Hebu fikiria ubaguzi uliopo kati ya wazungu na waswahili. Hivi, ukimpeleka mtoto akadhalilishwa utamlaumu nani?

Nne, tunapoamua kuwapa watoto wetu elimu tuhakikishe tunafanya hivyo bila kuwapora haki nyingine kama vile kulelewa na wazazi wao. Nakumbuka kisa ambacho rafiki yangu alinitaarifu kuwa alikuwa akimtuma mtoto wake kwenye kusoma shule ya msingi nje ya nchi. Badala ya kufurahia na kumpongeza, nilikasirika na kumpa pole. Nilimuuliza swali moja tu. "Hivi mtoto wako akidhalilishwa safarini au shuleni utamlaumu nani?" Hii ilikuwa ni baada ya kumuuliza namna anavyomsafirisha mtoto huyo kwenda nchi jirani. Alijibu kuwa alikuwa amemwamini mtu mwingine kumpeleka. Hapa ndipo swali la uwezekano wa udhalilishaji lilivyoibuka. Kufupisha kisa hiki, jamaa alimrejesha mtoto wake nchini na kumsomeshea nyumbani. Je ni wazazi wangapi wanashindwa kuona haya kwa sababu ya kuangalia tu elimu na lengo zuri la kuitoa?

Tano, je, tunahitaji shule za bweni kweli au ni biashara ya kuuza elimu na huduma ya malazi ambayo kimsingi, kwa shule za msingi haihitajiki hata kidogo? Kwa wale waliosoma miaka ya 80 hadi 2000 ni mashahidi kuwa mambo ya shule za bweni za msingi hayakuwepo nchini. Ila baada ya kuja kwa uhuria wa kila kitu, kuna vitu tunavifanya bila kuzingatia hatari au madhara yake hasa kwenye dunia hii iliyobadilika sana.

Bila kupendelea, nimetaja shule iliyohusika na mkasa si kwa kuichukia bali kuitumia kama mfano. Kama taifa, tunapaswa kutafakari upya namna tunavyotoa baadhi ya huduma. Tukianzia na elimu, sidhani kama ni busara kuwa na shule za msingi za bweni sawa na ambavyo si busara kuwa na mabaa na nyumba za chap chap karibu na shule ziwe za msingi hata sekondari. Naamini ustawi wa jamii watakuwa wameshtuliwa na msiba tajwa kiasi cha kujiuliza kwanini hawakuliona hili. Kumtoa nyumbani kwa wazazi wake katika umri ambao anahitaji malezi yao ni kumdhulumu haki ya kulelewa na wazazi. Mtoto wa umri tajwa anahitaji malezi, mapenzi na usimamizi wa wazazi. Nje ya mada, ndiyo maana mtoto akilazwa hospitali, kitu cha kwanza ni kutakiwa kuwa na mtu wa kukaa naye kutokana na utegemezi wake.

Tumalizie. Tunaomba mamlaka husika na jamii kwa ujumla kuliangalia upya hii kadhia ya shule za bweni msingi. Tuonane wiki ijayo ambayo tutaangalia harakati za uchaguzi.

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO



Na Joseph Kulangwa

# Bongo na siasa zake ni balaa!

UKIFANIKIWA kuishi Tanzania miaka mingi, usipofanikiwa kuwa kichaa, basi utakuwa msanii tu kwa vyovyote. Na kuwa msanii si lazima ukaigize majukwaani au luningani, redioni au hata kwenye kumbi za starehe.

Unaweza kujikuta msanii ukiwa na familia yako nyumbani kwako. Watoto ndio wataweza kubaini kuwa huyu baba au huyu mama, tayari zimemruka au ameshaingia katika kundi la maigizo au futuhi au komedi.

Utakuwa unajisemeasemea mwenyewe au hata kupiga teke makopo na mawe yanayokuwa mbele yako, wewe ukidhani ni burudani yako, lakini kumbe unawakwaza wenzio. Ukishamaliza hiyo unaingia ngazi nyingine sasa, unakuwa mwanasiasa.

Ukishakuwa mwanasiasa, utaanza kusema ya uongo na ya kweli. Kuna wakati utazidisha ya uongo na ukibaini umegundulika, ndipo utaanza kusema ya ukweli ingawa kwa kiwango kidogo sana.

Utasikia mtaani watu wanaanza kulalamika kuwa kumbe siasa si hasa, na ukitaka kuwa mwanasiasa lazima ujiandae kusema uongo, ndipo utakubalika na wengi. Ukitaka kuwa mwanasiasa, lazima ujiandae pia kuwa mwigizaji, uwe msanii.

Mwaka huu tulishuhudia wasanii wengi wakiingia kwenye kinyang'anyiro, baadhi wajumbe wakawapiga spana na wengine lakini wachache sana wakapenya, na sasa wanahangaika majukwaani kukampeni, huku wakichanganya na usanii.

Hawa ni wale wanaovutia wapiga kura kwa kuwaimbia nyimbo, kwa sababu wana kipaji cha kuimba, wasio na kipaji ndio wale wanaoongopa sana, mpaka washangiliwe na kupigiwa makofi. Wakiona hawaridhiki utawasikia wakihoji: "Wangapi mtanipigia kura, mikono juu?"

Hebu tazama picha hili; ni mfano tu msijenitoa macho, wanaomwunga mkono mgombea wa chama tawala, wanafanya hivyo wakitaja maendeleo aliyowaletea katika kipindi chake cha kwanza cha miaka mitano.

Wanamwunga mkono wakitaka apewe mingine kama hiyo, kwa sababu ya miradi aliyojenga. Wanataja kama anavyoitaja yeye. Amejenga reli ya kisasa, barabara za juu Dar es Salaam, bwawa la mitambo ya kuzalisha umeme, barabara kila mahali, umeme karibu kila kijiji, ndege za kumwaga.

Si uongo, hayo ameyafanya na kila mwenye macho haambiwi tazama. Lakini miradi hiyo hiyo inatumiwa na wengine wa upinzani kumpinga, tena wanaitaja hivyo hivyo, wanakiri ipo, lakini wanaitumia kumpinga!

Wakati yeye na kambi yake wanasema tumeweza kujenga miradi hiyo kwa fedha zetu wenyewe, wanaompinga wanasema kodi hiyo imetumiwa vibaya ni afadhali ingekwenda kwenye mishahara, ili mifuko ya watu ijae watu wale ubwabwa.

Akiwaambia tumejenga na kupanua viwanja vya ndege, wao wanaibuka na kusema ndiyo, mbona vingine havina faida na kwa nini umevijengea huko na si huku? Utadhani viwanja hivyo hazitui ndege, zinatua na haohao wanazipanda. Ndiyo, lazima wazipande kwa sababu wanasema ni kodi yao na hawana mbawa waruke wenyewe.

Sasa kama ni kodi yao ubaya uko wapi kuzinunua? Hawakosi majibu lakini, watayachakura kwenye mafaili na kuibuka wakisema mbona wakati unazinunua hukutwambia. Na wengine utawasikia wakisema hivyo na baada ya muda wanafanya bukingi ya kwenda Mwanza.

Hapo ndipo unaweza kuwajua Watanzania, na kwa kweli wanafurahisha na ukiwafuatilia saana ndipo nawe maisha yako yanazidi kurefuka, kwa sababu utakuwa unacheka tu na kupata furaha pekee unayoweza kuipata.

Hizo ndizo siasa zetu Wabongo, lakini jua kwamba kipindi hiki kikipita salama, basi tunasahau na kuwa wamoja. Tunasahau kabisa kauli tulizotoa kwenye kampeni za kuondoana kwenye reli hivihivi!

Tanzania au Bongo, kwa kweli raha sana, huyu akitaka alete maendeleo huyu anatia mguu anahoji kwa nini. Huyu akisema jamani maendeleo hayana chama, lakini nichagulieni mafiga matatu, huyu anatoa macho akisema haelewi.

Anataka kujua mafiga matatu kivipi wakati figa moja linaweza kuwa bovu, au hata mawili na moja ndilo likawa na uwezo wa kubeba sufuria la maji! Lakini ndio mchuano huo, akili mukichwa kwa wanaopiga kura, vinginevyo nao watalokota makopo kumitaa. Wengine hubebwa na kauli ya mafiga tu hawana uwezo. Alamsiki!

KONA YA UKWELI

# Mchakako kura za maoni CCM usiwagawe Kyela



Na Thobias Mwanakatwe

KIPYENGA cha kampeni kwa ajili ya uchaguzi mkuu unaotarajia kufanyika Oktoba 28, mwaka huu, kilianza kutimua vumbi rasmi Agosti 28, kwa wagombea walioteuliwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kunadi sera za vyama vyao ili kushawishi wananchi waweze kuwachagua.

Kila chama kimekuwa na utaratibu wake lakini kwa Chama Cha Mapinduzi (CCM) wanachama wake huomba kuwania nafasi ya uongozi. Mchakato wa kura za maoni kwa waombaji hufanyika na kisha vikao vya chama huketi kuteua jina moja la mwanachama atakayepeperusha bendera ya chama chake.

CCM, ambayo ni chama kikongwe nchini, kimekuwa na utamaduni wake wa muda mrefu katika kuwapata wateule ambapo hata kama mtu ameshinda kura za maoni si hakikisho la kuteuliwa kuwania nafasi uliyoomba, la hasha, kuna mambo mengi yanayoangaliwa kabla ya kuteuliwa.

Wakati majimbo mengine makundi ya kisiasa yaliyokuwepo wakati wa mchakato wa kura za maoni yalishavunjwa, hali ni tofauti kidogo katika majimbo jirani ya Rungwe na Kyela mkoani Mbeya kutokana na wateule na wapambe wao kushindwa kushuka ipasavyo na kuomba ushirikiano wa waliowatangulia.

Hali si mbaya sana Rungwe kwani mgombea, Anthony Mwantona, hana kauli mbaya dhidi ya Sauli Amon, Mbunge aliyemaliza muda wake, hivyo kukubalika kwake kunazidi kuongezeka siku hadi siku.

Mbali na makundi ndani ya CCM, anapambana na Mbunge wa Viti Maalum Chadema aliyemaliza kipindi chake, Sophia Mwakagenda, ambaye nguvu zake zitaendana na ukubwa wa mgawanyiko ndani ya CCM.

Kyela ni tofauti kidogo ambapo mgombea ubunge kwa tikiti ya CCM, Ally Mlaghila, hawezi kumaliza hotuba yoyote ile ya kampeni bila kumpiga vijembe Dk. Harrison Mwakyembe, mbunge aliyemaliza kipindi chake, hivyo kuimarisha makundi ndani ya CCM.

Wananchi wengi Kyela hawaoni sababu ya mwanasiasa huyo kutaka kujenga jina lake kwa kumshambulia majukwaani Mwakyembe ambaye, mtu atake, asitake, ameibadilisha Kyela kwa kiwango kikubwa.

Mwakyembe anatumia muda mwingi Mbeya Mjini kumsaidia Dk. Tulia Ackson alitwae jimbo hilo. Nilimuuliza kwa nini hagawi muda wake ili na Kyela asaidie. Akanijibu kuwa mgombea Kyela hahitaji msada wake, ananguvu ya kutosha kulitwaa jimbo hilo.

Lakini taarifa nilizopata Kyela ni kuwa Mlaghila hamtaki Mwakyembe kwenye kampeni zake kwa madai kwamba atamharibia. Wengine wanadai kuwa Mwakyembe akiwapo, staili yake ya kampeni ya kumshambulia mtangulizi wake, haitaendelea.

Vyovyote vile na iwe, CCM inajipalia mkaa Kyela! Tayari CHADEMA wameuona upenyo wa ushindi mapema!

Mgombea ubunge wa CHADEMA, Alinanuswe Mwalwange, amepata umaarufu kwa kusisitiza, kama Rais John Magufuli afanyavyo, kwamba maendeleo hayana chama, hivyo ampongeza sana Dk. Mwakyembe kwa kazi kubwa aliyoifanya Kyela na kuahidi kuwa atamalizia pale alipoishia.

CCM bado haijachelewa kurejesha siasa za kistaarabu Kyela, kwanza kwa kumfunda Mlagila na wapambe wake kuwa wanachezea moto. Pili kumfunda Katibu mpya wa CCM, Gervas Ndaki, kuacha kuchochea makundi ndani ya chama hicho.

Hatua aliyochukua Jumapili iliyopita ya kumwondoa Katibu Kata wa Makwale, Ipyana Mwangunga, kwenye ukurugenzi wa uchaguzi wa Kata yake, kwa madai kuwa ni msaliti na mpambe wa Mwakyembe ni utoto uliopindukia na ni kuendeleza makundi.

CCM Mkoa wa Mbeya na Wilaya ya Kyela isisahau karipio la Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan alipotembelea Kyela wiki tatu zilizopita kwa "wenye vidomodomo vya ufitinishi" kwamba waache mara moja katika kipindi hiki cha Uchagu Mkuu. Ujumbe kama huu alitoa Rais Magufuli alipotembelea Wilaya ya Kyela mwezi Aprili mwaka jana kuwa Kyela ina majungu!

Binafsi, niwaombe viongozi, wanachama na wapenzi wa CCM Kyela, kipindi hiki ni cha kunadi Sera na ilani ya chama siyo kuanza kulumbana kudhalilisha, acheni tofauti zenu.

Viongozi wa Chama Wilaya mjikite zaidi kukipigania chama kiweze kuibuka na ushindi badala ya kutumia muda mwingi kuandika barua na kusema fulani ni msaliti.

Nachofahamu makundi yalishavunjwa baada ya chama kuteua jina la Mlaghila kuwania ubunge Kyela, lakini nachokiona hapa viongozi wa chama ndani ya wilaya ndio wanaendekeza fitina, umbeya na majungu ambavyo havisaidii chama.

Ifahamike kuwa haya niliyoyoandika ni maoni na mtazamo wangu mimi.

***MUNGU IBARIKI TANZANIA, MUNGU IBARIKI KYELA.***

***Kwa maoni na ushauri tuma; Email: mwanakatwe2015@gmail.***

DARASA LA NDOA

# Umuhimu wa kutambua haiba yako katika kuimarisha ndoa



Na Mch. Dk. Enock Mlyuka 0744000066

PAMOJA kwamba sote tu wanadamu, lakini kila mwanadamu ana tabia na hisia zake za kipekee zinazomtambulisha kuwa yeye ni mtu wa aina gani. Tabia na hisia hizo za kipekee huitwa haiba.

Kila mwanadamu ameumbwa akiwa na mwelekeo fulani, uwezo na udhaifu wa asili wa aina mbalimbali. Baadhi ya watu wamezaliwa wakiwa na mwelekeo wa ucheshi, upole, ukali, ukimya, uzungumzaji na kadhalika.

Migogoro mingi katika ndoa inachangiwa na wanandoa kutokutambua vizuri kwa nini wenzi wao wako jinsi walivyo. Pamoja kwamba tabia za asili ni vigumu kubadilika, zinaweza kudhibitiwa.

Ni muhimu sana kwa wanandoa na watu wote kufahamu haiba ya mtu mwingine. Ufahamu huo unasaidia kujua namna ya kuishi, kuchukuliana na kushirikiana na mtu mwingine katika mazuri au upungufu wake. Hali hiyo husaidia pia kuepusha migogoro isiyo ya lazima katika ndoa na maeneo mengine katika jamii.

Kwa wale ambao hawajaoa au kuolewa, mada hii itawasaidia kuwa na matarajio ya aina fulani ya tabia inayoweza kujitokeza kwa mwenzi baada ya kuoa au kuolewa. Haiba huathiri jinsi mtu anavyofikiri, anavyojisikia na kujiheshimu. Watu wakizikubali na kuzielewa tofauti zao watajenga uhusiano imara.

Wanasaikolojia wamegawa haiba katika makundi manne ambayo ni Melankoli (Melancholic), Flegmatiki (Phlegmatic), Sangwini (Sanguine), na Koleriki (Choleric).

Kundi la Melankoli Neno Melancholy linamaana ya -enye huzuni au enye uzito wa moyo. Kwa kawaida, watu katika kundi hili sifa yao kuu ni upole na ukimya.

Kwa maneno mengine, hawapendi kuongea mbele za watu wengi; kwa sababu ya ukimya wao, si rahisi kujua wanawaza au kufikiri nini, si rahisi kuwazoea au kuzoeleka kwa haraka; hawapendi kuchangamana sana na watu wengine, hivyo si wepesi kutengeneza marafiki.

Pamoja na ukimya wao, hawa ni watu wenye hasira kali inayodumu kwa muda mrefu, hivyo, si wepesi kusamehe an kuomba msamaha.

Melankoli ni watu wenye hisia za ndani sana ya moyo, hivyo, wakipenda wanapenda haswa, wanampenda mtu mzima mzima, lakini wakichukia, wanamchukia mtu haswa haswa.

Watu wa aina hii huumia sana moyoni wanaposalitiwa au kuumizwa; ni watu wepesi kukasirika au kukwazika. Yaani ukimkwaza kidogo tu, anakuondoa moyoni, ndiyo maana huwa ni wagumu kumwamini mtu haraka kwa kuhofia kuumizwa.

Ni watu makini, wachambuzi na wakosoaji sana wa watu wengine hasa kutokana na tabia yao ya kujali mambo madogo madogo.

Hali hii imesababaisha baadhi ya wanaume hasa wanawake kuchukua muda mrefu sana kupata watu wa kuwaoa au kuolewa nao au kuamua kutokuolewa kabisa. Kwa upande wa tendo la ndoa, hawavutwi kufanya tendo la ndoa mara kwa mara.

Melankoli wanaweza kuoa au kuolewa na Sangwini pamoja na tofauti walizo nazo. Kinachoangaliwa kati yao ni upya utokanao na tofauti zao.

Kwa kuwa, Melankoli wana tabia ya upole, hivyo ni rahisi 'kushuka' pale wanapoudhiwa na 'Sangwini', ambao wana tabia ya 'kupanda' juu kwa hasira kunapotokea kutofautiana katika jambo fulani.

Melankoli wanaweza kuoa au kuolewa na Koleriki, watu wenye hasira. Melankoli wanaweza pia kuoa au kuolewa na Flegmatiki, watu wenye ujasiri na sifa nyingi zinazofanana.

Jambo la msingi, Melankoli hupenda ndoa na siyo kuchezeana tu. Wanahitaji mtu makini, anayejiheshimu na mwenye msimamo. Pia, wanahitaji mtu aliyejitoa kwa ajili ya maisha ya familia. Kwa ujumla, Melankoli anaweza kuoa/kuolewa na mtu kutoka makundi yote.

Flegmatiki (Phlegmatic)

Neno phlegm linamaana ya utulivu, upole. Hawa ni watu wenye hisia sana. Wanapotafuta mtu wa kuoa/kuolewa naye, Flegmatiki, hutazama zaidi wenye akili na hisia zinazokaribiana au kufanana.

Kwa mtazamo huu, ni rahisi kwa Flegmatiki kumwoa Flegmatiki mwenzie kuliko makundi mengine ya haiba. Hata hivyo, hii haina maana kuwa Flegmatiki hawezi kuoa/kuolewa na makundi mengine.

Kwa kawaida, Flegmatiki kupenda, kwake ni suala la uhusiano wa kudumu (ndoa), hivyo, wana kawaida ya kutafuta wenzi kwa ajili ya kuwa kiunganishi, kukuzana na kupatana.

Kwa kuwa Flegmatiki ni watu wenye hisia sana, hupendelea sana simu pamoja na njia nyingine za kielektroniki ili kuchambua uhusiano wao. Kwa hiyo, mtu akiwa na mwenzi aina ya Flegmatiki, anapomtumia ujumbe wa simu anafurahi sana na pengine hawawezi kufuta ujumbe wenyewe hata kama umepitwa na wakati. Kwa kuwa, kupitia mawasiliano ya aina hiyo, Kwa Flegmatiki ni rahisi kutambua malengo na fikra za wenzi wao.

Sifa za ziada za Flegmatiki si wazungumzaji sana, lakini watu wenye furaha muda mwingi. Wanafurahia kuona watu wakicheka; na wakati mwingine wanaweza kusema kitu cha kuchekesha, lakini wao wasicheke.

Si watu wa kukasirika haraka; Ni rahisi kuendana na watu wenye tabia mbalimbali. Hupenda kumfurahisha kila mtu. Ni watu wanaopenda amani mara zote; Kwa msingi huu, hawapendi kupinga au kukosoa.

Flegmatiki hawapendi kuona mtu amechukia au wao kuwa chanzo cha maudhi; huwa na uwezo mdogo wa kufanya uamuzi kwa sababu ya hali yao ya kupenda kumfurahisha kila mtu na kutotaka kuonekana mbaya.

Flegmatiki wanaweza kuoa au kuolewa na Sangwini ili kupata upendo wa kweli, lakini kwa wakati huo huo wakihitaji watu wacheshi. Wakati mwingine, Flegmatiki huoa au kuolewa na Koleriki ili kupata uwiano mzuri katika uhusiano. Kwa ujumla, Flegmatiki wanathamini ndoa na pia ndio lengo lao kuu la kuingia katika uhusiano.

Hata hivyo, wanapogundua wenzi wao hawaendani nao, wao huwaacha na kutafuta wengine. Kutokana na tafiti za wanasaikolojia, Flegmatiki huweza kuoa/kuolewa na Flegmatiki wenzao huku wakiishi vema kwenye ndoa.

# MAISHA

OKTOBA 11, 2020
Nipashe

Baba, Mama na Mwana

Jumapili




Ukurasa 14

**Scones za maboga, nazi na maziwa**



Ukurasa 15

## MAISHA NI NYUMBA

Sakafu yako ya jana yaweza kuwa muujiza wa leo



## HARUSI

Ukurasa 12



# 'BABY FACE' Sura isiyozeeka haraka

Ukurasa 14

# Katika umri huu mtoto hujua zuri, baya

Na Moses Ismail

NI kawaida, kwamba katika umri wa kuanza kutambaa hadi miaka miaka mitano, tunawachukulia watoto wetu kuwa hawajui zuri wala baya katika matendo yao wanayofanya.

Tunawaita jina zuri tu la'malaika' tukimaanisha hawajui lolote na hawawajibiki sana katika yale wanayoyafanya tukiamini hulifanya bila kujua uzuri au ubaya wake.

Kwa sababu hiyo, watoto wa umri huo hatu waonyi kwa 'ukali sana' kwa yale anayoyafanya, tunawachukulia poa tu tukisema; "ni utoto tu, akikua ataacha". Bahati mbaya wapo wanaokua na tabia zao za utoto ambao hawakatazi ki tena pale wanapofanya ukorofi katika umri usiopaswa kufanya tena ukorofi. Wanakuwa manunda!

Idadi ya watoto hao, manunda, ni kubwa na hiyo inasababisha malalamiko ya kuwepo kwa watoto watukutu katika jamii.

Hili linajenga swali la msingi, kwamba umri hasa wa kumfundisha mtoto tabia njema kwa kumfundisha kuwajibika kwa tabia zake ni upi?

Kwa elimu ya tabia ya asili ya mwanadamu, inaonyesha kwamba mtoto huanza kupokea mafunzo ya mema na mabaya tangu akianza kutambaa tu na hujifunza 'kuwajibika' kwa kufuatilia makatazo ya wakubwa zake kwa kila analolifanya.

Kwa mfano, chukulia mtoto huyo anayetambaa, katika kutambaa kwake anaelekea kwenye sufuria iliyowekwa maji, lakini kabla hajaifikia sufuria hiyo anageuka na kukutazama wewe mzazi wake usoni.

Mnapokutanisha macho yenu, anakuangalia kwa makini na kusoma kinachoongewa na uso wako, anapogundua kuwa hutaki aendelee kutambaa kusogelea sufuria hiyo anaamua kujichekesha na kufanya jambo jingine kabisa tofauti na kuifuatilia sufuria hiyo.

Na iwapo kama utakuwa makini na tendo hili la mwanao asiyezidi miezi tisa utagundua kuwa kwa kila jambo analotaka kufanya, katika mazingira ya karibu yako, basi ni lazima ageuke na kuangalia uso wako kabla ya kuamua kufanya ama kuacha.

Unaweza kuonyesha dalili zote za kumkataza asisogelee sufuria hiyo, kwa kumtazama tu, lakini akajaribu kulifuata ili apata uhakika kama uso na macho yako yana maanisha kweli anachokiona?

Katika hali hiyo, mzazi utatoa sauti ya 'acha' au 'rudi hapa', pia atakuwa makini kuliko wewe kwa kusikiliza sauti hiyo, akiona ina upole na haina msisitizo au taharuki, basi atajichekesha na kuendelea na mambo yake.

Hii ndiyo saikolojia ya watoto 'wachanga' wanapoanza kujifunza ni lipi zuri la kufanya na nilipi baya analotakiwa asilifanye. Ni hatua muhimu sana katika kumjenga mtoto kitabia.

Unapomjengea mtoto misingi ya kujua la kufanya au la kuacha katika umri huu, unamfanya awe mwepesi wa kusikiliza na kuwa na adabu na wala aihitaji kiboko ili kumfanya atii kile anachotakiwa au asichotakiwa kufanya na hili uganda katika ubongo wake hadi ukubwani.

Kwa kumtengeneza mwanao akiwa katika umri huo wa kutambaa kwake, miezi saba au tisa ya mwanzo ya maisha yake, ni jambo muhimu na linalopaswa kufanywa na kila mzazi kwa mustakabali wa kuwa na tabia nzuri na mwenye kusikia.

Usichukulia kabisa kwamba kile anachokifanya mwanao huku akiwa anakutizama usoni kama ni kitu cha kitoto, hapana. Anapokuangalia usoni ni kwamba anajaribu tu kujiridhisha kwa akili yake ya tabia za maumbile kama anachofanya ni sawa au si sawa.

## QUIZ

NA KHAMIS KIDAGO 0657 207168

**MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA**

**1.** Bainisha kama maneno yafuatayo ni Masculin au Féminin.

Mfano: Ballon rond – Masculin.

- Définition précise – F
- Chanson espagnole – F
- Don généreux – M
- Leçon intéressante – F
- Liaison incorrect – M
- Feuilleton mensuel – M
- Action particulière – F
- Crayon noir – M
- Façon élégante – F
- Maison ancienne – F
- Inscription definitive – F
- Rayon lumineux – M
- Son aigu – M
- Wagon plein – M
- Caleçon léger – M
- Habitation curieuse – F
- Balcon fleuri – M
- Saison froide – F
- Savon doux – M
- Joli visage – M
- Petit message – M

**2.** Pigia mstari kivumishi kinachoendana na kila sentensi zifuatazo.

i. Pourquoi as – tu mis ce pantalon BLANC (blanc – blanche)?

ii. Il m'a donné une réponse FAUSSE (fausse – faux).

iii. C'est vraiment un acte FOU (fou – folle).

iv. Je voudrais une boisson FRAICHE (fraîche – frais) s'il vous plait.

v. Quelle jolie chatte ROUSSE (roux – rousse) !

vi. J'adore conduire cette VIEILLE (vieux – vieille) voiture.

vii. Ce parfum est vraiment DOUX (doux – douce).

viii. Pourquoi est – t – elle si JALOUSE (jaloux – jalouse)?

ix. J'ai envie FURIEUSE (furieux – furieuse) de lui voir.

x. Quelle MAUVAISE (mauvais – mauvaise) odeur!

xi. C'est un homme très AMBITIEUX (ambitieux – ambitieuse).

xii. Beatrice est une fille COURAGEUSE (courageux – courageuse).

xiii. Ce soir il y aura une soirée DANSANTE (dansante – dansant).

xiv. Voilà un BON (bonne – bon) endroit.

xv. L'eau COURANTE (courante – courant).

**Le quiz du week – end**

1. Nyumbua kitenzi **"Être"** kama maelekezo yanavyoonesha hapo chini.

Conditionnel

Présent

| | |
|---|---|
| Je | serais |
| Tu | serais |
| Il/elle | serait |
| Nous | serions |
| Vous | seriez |
| Ils/ells | seraient |

Passé

| | | |
|---|---|---|
| J' | aurais | été |
| Tu | aurais | été |
| Il/elle | aurait | été |
| Nous | aurions | été |
| Vous | auriez | été |
| Ils/elles | auraient | été |

**2.** Nyumbua kitenzi "Être" katika "Infinitif" présent na passé.
- Présent = être
- Passé = avoir été

**3.** Weka kitenzi "Être" katika Participe présent na passé.

Présent = étant
Passé = été
ayant été

**4.** Pangilia kitenzi "Être" katika Impératif présent na passé.
Présent = sois
soyons
soyez


Passé = aie été
ayons été
ayez été

## WATOTO

## PAKA RANGI



## CHEKA



Alichokifanya daktari

SIKIA panya hawa watatu wanavyobishana

**Panya wa kwanza**: Jamani mimi baba lao, wiki hii nimekula sumu mara tatu, bado nadunda

**Panya wa pili:** Wewe unasema nini? Mimi nimekula nyama ikiwa kwenye mtego mara tano, lakini sijawahi kudakwa.

**Panya wa tatu:** Mmemaliza kujigamba? Mimi ndio mwamba, hapa nilipo nimebeba mimba ya paka !!!

SWALI
Tanzania kuna bandari ngapi kubwa?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Mwanamume anafanya kazi lakini mkewe kutwa anazurura mitaani

MPENZI msomaji, wakati unatafakari makala iliyopita kuhusu wale kinababa wanaowapiga wake zao hadi kuwaachia makovu, huku wengine wakiua kabisa, leo nigusie kidogo wanawake wasiotaka kujishughulisha, lakini kutwa nzima wanazurura na kuwaachia waume zao wakitafuta riziki ya familia.

Wako wanawake ambao baada ya kuolewa hujiona ndio wamefika. Badala ya kubuni miradi ya kujipatia kipato, wao huanza kutafuta vijisafari vya hapa na pale kuwatembelea ndugu na marafiki, huku mume akichakarika kutafuta riziki.

Ukiona mwanamke wa aina hii, ujue tabia hiyo amekuwa nayo tokea akiwa kwa wazazi wake, ameizoea. Anasahau kwamba ameshaingia katika utaratibu mwingine wa maisha ya kutulia ajenge familia yake. Anaona watoto wanaongezeka lakini hajiulizi mahitaji ya watoto yanapatikana vipi.

Wapo wanawake ambao waume zao hubuni na kuwaanzishia miradi ya kufanya lakini kutokana na uvivu hujifanya hawawezi kusimamia. Wanawake wa aina hii ndio wale wenye tabia ya kuwakalia waume zao vichwani.

Yawezekana mume ni mpole, hataki shari na kazi yake ndiyo inayomchukulia muda wake mwingi. Na zaidi mwanamke anapogundua udhaifu wa mumewe, eti kwamba anampenda sana, au hawezi kumwambia kitu, ndipo anapozidisha uonevu na kujigamba kwamba hawezi kuguswa.

Wanawake wa aina hii ni hatari sana. Hawa ndio hata wanapoachwa nyumbani, hutumia mwanya huo kufanya vituko nyumbani, ikiwa ni pamoja na kuleta nyumbani wageni, marafiki hata majirani pasipo mpangilio.

Wengi wenye tabia hii wamejikuta wakihaha baada ya ama kulizwa na marafiki zao au wakizihama nyumba zao baada ya mume kuchoshwa na tabia za ajabu ajabu na kuishia kutimuliwa.

Wanawake wa sampuli hii, ukiwachunguza unaweza kugundua kwamba hata maisha yao ya awali hayakuwa ya kimaadili. Hebu msomaji nikupe mfano mmoja niliyesimuliwa na jirani yangu.

Anasema, yupo mama mmoja alifukuzwa na mumewe, kisa ni kiruka njia pale mumewe awapo kazini. Mara kadhaa mume anarudi nyumbani kwa kushtukiza na kumkosa mkewe hayupo.

Akimuuliza pale anaporejea hujitetea kwamba alikwenda kusalimia ndugu zake au alikuwa kwa jirani. Wakati huo mama huyu anapokuwa hayupo nyumbani, watoto wao watatu wanakuwa shuleni. Watoto wawili wapo shule ya msingi na mmoja na mkubwa kidato cha kwanza.

Jirani yangu huyu akaniambia kuwa tatizo la mama huyo ni kwamba mumewe alimpata kwenye vilabu vya pombe kama mhudumu, alipompenda akamchukua kuishi naye.

Awali mama huyo alikuwa na adabu na heshima. Kwa tabia hiyo, ilimfanya mwanaume wake aamue kwenda kufunga naye ndoa kanisani baada ya kuzaa watoto hao watatu.

Tangu kufungwa ndoa hiyo, ndipo mwanamke huyo alipoanza kubadilika, hatulii nyumbani, hawatembelei tena wakwe, amewasusa akiwatuhumu wachawi, huku akimnyanyasa mume wake.

Hata hivyo, mume wake tayari ameshtuka baada ya kumweke mitego ya kurudi nyumbani kwa kushtukiza. Niliwahi kuambiwa na rafiki yangu mmoja kwamba, mtu anayetoka sehemu ya shida na akapata penye neema, hujidai huku akisahau alikotoka.

Mpenzi msomaji, labda ushauri mdogo tu kwa kinababa; kwamba katika miaka ya hivi sasa, msiwaruhusu wake zenu wawe mama wa nyumbani pasipo kujishughulisha. Watafutie kitu cha kufanya hata kama ni kwa lazima ili mradi anachangia pato la familia.

Siku hizi, imedhihirika kwa kiwango kikubwa kwamba wanawake ni wajasiriamali wazuri hata kuliko kinababa. Hawa ni wasimamizi wazuri wa miradi, waratibu na wachumi wazuri. Msikubali wake zenu wakae tu nyumbani.

Utafiti unaonyesha kuwa wanapoachwa nyumbani bila shughuli inayowaingizia kipato, ndio hao wanaoishia kuwa viruka njia na kusababisha mfarakano ndani ya familia. Wanapoachwa kuzurura wanapata mwanya kufanya maovu ikiwa ni pamoja na kushawishika kuwa na uhusiano nje ya ndoa.

Tukumbuke, zipo hasara kama vile watoto nje ya ndoa, na zaidi ya yote magonjwa mabaya mfano UKIMWI. Kinababa zinduka wajanja ni wengi msipodhibiti wake zenu. Maisha Ndivyo Yalivyo.

Bila shaka msomaji umejifunza jambo hapo. Wiki ijayo nitajadili wale wanaume wanaopiga vita wake zao walioko tayari kazini au wanaotaka kufanya kazi wanawazuia.

***Je, una maoni au jambo ungependa tujadili pamoja? Nitumie kupitia ujumbe mfupi kwenye 0715268581. Pia namba hii ipo WhatsApp. Tukutane wiki ijayo.***

## NAWAZA KWA SAUTI

Na Salome Kitomari



# Tukiwapata kina Mtaka 30 mikoa itapaa kimaendeleo

KWA muda mrefu nimekuwa nikifuatilia harakati za Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Anthony Mtaka, ambaye nina uthubutu wa kusema ni kiongozi wa kuigwa na viongozi wa aina yake na wengine wanapaswa kwenda kujifunza.

Upo usemi usemao mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni. Leo nawaza kwa sauti imejikuta mkoani Simiyu na kuwaza iwapo wangekuwepo kina Mtaka 30 maana yake kila mkoa ungekuwa na mambo makubwa na mazuri hasa yanayogusa maisha ya watu moja kwa moja.

Hakuna ubishi kuwa wako baadhi ya viongozi wa mikoa hii wanafanya kazi nzuri sana za maendeleo lakini bado hawajafikia anayoyafanya Mtaka ambayo yanastahili kuigwa.

Kiongozi huyu amekuwa mbunifu na kuinua kiwango cha ufaulu kwa kufanya mambo ambayo yanawezekana kwingine. Kutokana na kazi zake, ameendelea kuuweka mkoa huo kwenye ramani za 10 bora, ikiwa ni mkoa mpya.

Nikitoa mfano wa karibuni, juzi katika ukurasa wake wa Facebook na vyombo vya habari, alitoa taarifa ya namna mkoa umejipanga kuhakikisha wanakuwa na ufaulu mzuri.

Aliandika kuwa viongozi wa mkoa walikutana na wanafunzi wanaojiandaa na mitihani ya taifa darasa la saba kwa ajili ya kujiridhisha na maandalizi pamoja na kuwatakia heri na kutamka zawadi za mwaka huu.

Zawadi zilizotangazwa ni wanafunzi watakaoingia 10 bora kitaifa kila mmoja atapewa Sh. 500,000, mwalimu atakayeongoza kwa ufaulu wa alama A nyingi kimkoa atapewa Sh. 500,000 (masomo matano na kila moja Sh. 500,000).

Aidha, shule itakayoingia 10 bora kitaifa alimu wake wote ataenda ziara ya utalii katika Hifadhi ya Taifa Serengeti.

Katika matokeo ya mwaka 2019 Mkoa wa Simiyu ulifaulisha watoto wanne waliingia 10 bora kitaifa kwenye shule za serikali na kila mmoja alipewa Sh. 300,000.

Hii ni motisha kubwa sana kwa walimu na wanafunzi, kwanza mbali ya kiasi cha fedha watakachopewa lakini wataona wamethaminiwa na kiongozi mkuu wa mkoa wao, na wataongeza motisha.

Katika kutimiza wajibu wowote ule inapotokea mwingine wakathamini huongeza morali ya kile kinachofanywa, mathalani walimu wataona wamethaminiwa sana na licha ya changamoto za kazi lakini wataongeza bidii, atajiona ni wenye deni moyoni.

> **“Kwa sasa tunaona makongamano na mikutano ya kitaifa inafanyika mkoani Simiyu, hiyo ni kutokana na jitihada zilizoonyeshwa na kiongozi huyo ambaye ameifanya Simiyu kuwa katika ramani za juu za taifa.**

Vivyo hivyo kwa wanafunzi ni wajibu wao kusoma na kufaulu, lakini kiongozi wao anapoonyesha kuwathamini basi bidii huongeza.

Wataalam wanasema morali ya kazi au kitu chochote haitokani na mshahara mtu anaolipwa au wajibu anaotekeleza mhusika kutokana na kazi au wajibu, bali kumjali ni tiba ya moyo wowote.

Nakumbuka kuna miaka Manispaa ya Moshi ilianzisha utaratibu wa kuwazawadia wanafunzi wanaofanya vizuri ikiwa ni pamoja na kuwatambua walimu wao. Hatua hii ilisaidia sana na Manispaa hiyo ilikuwa katika nafasi za juu kitaifa kwa kufaulisha.

Chini ya uongozi wa Mtaka, zimeanzishwa kambi za kitaaluma ambazo wanafunzi hukaa kwa zaidi ya siku 60 na hutembelewa na viongozi mbalimbali na watu waliofanikiwa, ambao huzunguza nao ili kuwapa hamasa ya namna ya kufanya vizuri zaidi.

Watu maarufu au wenye mafanikio wanaoalikwa kwenye kambi hizo hutia hamasa kwa wanafunzi hao kufanya bidii ili kufanikiwa, lakini hujifunza safari ya mafanikio ya muhusika, njia alizopita ambazo wakati mwingine ni ngumu na mwisho alivyoruka viunzi vyote na kufanikiwa.

Huu ni ubifuni huo mkoa huo umeendelea kupaa kila uchao, mathalani katika matokeo ya kidato cha sita ulishika nafasi ya tatu kitaifa na zilitolewa zawadi kwa walimu na wanafunzi.

Jitihada zingine zinazoonekana ni katika kuvutia wawekezaji kwenye viwanda kama vya nguo na vyombo vya udongo na tayari walishapata mwekezaji ambao watatumia malighafi za mkoa huo na kutoa ajira kwa wananchi.

Kwa sasa tunaona makongamano na mikutano ya kitaifa inafanyika mkoani Simiyu, hiyo ni kutokana na jitihada zilizoonyeshwa na kiongozi huyo ambaye ameifanya Simiyu kuwa katika ramani za juu za taifa.

Kama haitoshi kwa sasa maadhimisho ya siku ya wakulima (nane nane) yanafanyika kila mwaka katika viwanja vya Nyakabindi mkoni Simiyu, ambayo maelfu ya watu huchangia uchumi wa mkoa huo, na fursa ya elimu kwa wananchi.

Kwa uongozi wake sasa tunaona Simiyu mpya ambayo haina umri mkubwa, lakini mambo yake ni makubwa kwa kuwa kuna kiongozi sahihi na ni wakati kwa viongozi wengine kujifunza kwa kinachofanyika.

***Mungu ibariki Tanzania***
***Mungu Ibariki Afrika***
***Kwa maoni, ushauri: salomekitomari33@gmail.com***

# HARUSI








Maharusi wetu leo ni Hamphrey Shao na Ndenisia Mbowe, waliofunga ndoa, Septemba26, 2020 katika Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Usharika wa Keko, jijini Dar es Salaam.



# MITINDO







## RAHA YA KIJORA

NGUO aina ya vijora inahusishwa na matukio mengi ya sherehe, lakini kwa ujumla ni vazi zuri ambalo wanawake wakivaa wanapendeza.

Katika sherehe nyingi na matukio ya misiba, wanawake wanaonekana wakivaa vijora kama vazi rasmi.

Hata katika maduka ya nguo, vijora vinauzwa kama sare maalumu na wanunuzi wakuu ni wale watu wenye kuandaa shughuli mbalimbali.

Lakini uvaaji wake ndio unawashangaza wengi, kwani kutokana na vazi hilo kuwa kubwa na nyepesi, mtu hulazimika mkono mmoja kushikilia nguo ili kumudu kutembea vizuri.

Kutokana na aina hiyo ya uvaaji, ndipo ndipo umeibuka ule msemo kwamba 'Raha ya kijora, lazima ushikilie'.

Hata hivyo, vazi hili ni moja ya nguo zilizoundwa kiheshima zaidi kama ilivyo kwa Madira au baibui.

Wapo wabunifu ambao wameanza kushona aina tofauti ya vijora ili kuwafanya watu wengi kuvutika na kuvaa kwa heshima.

Kwa ujumla nguo hizi zinapovaliwa vizuri mtu anaweza kwenda nayo ofisini, matembezini na kwenye hafla mbalimbali.

# UREMBO



## 'BABY FACE'

# Sura isiyozeeka haraka

KUNA baadhi ya wanawake wamebahatika kuwa na sura ya kitoto ambayo kila wakati anaonekana kijana.

Hata kama umri wake unavyozidi kwenda mbele, lakini uso wake hauonyeshi kuchoka na badala yake unazidi kuwaka.

Watu walioumbwa na sura za aina hiyo kwa kawaida huwa na furaha wakati wote na kujiamini.

Hata hivyo, idadi ya wanawake wenye sura ya kitoto bado ni ndogo.

Wataalamu wa masuala ya urembo, wanasema idadi kubwa ni wale wenye sura zinazozeeka haraka, huku ikitawaliwa na alama za makunyazi.



Hata hivyo, kwa wenye hali hiyo hakuna haja ya kuwa wanyonge, kwani kuna njia mbalimbali ambazo ukizichukua unaweza kubaki katika hali ya ujana.

Wataalamu wa vyakula vya asili, wanasema kuna baadhi ya vyakula vinatoa matokeo mazuri endapo mtu akila kila siku au kutumia kama 'Massage' ya usoni.

Baadhi ya vyakula hivyo ambayo huwa vinaleta matokeo ya haraka ni pamoja na maziwa, kahawa na mchele.

**MATUMIZI YAKE**

Chukua maziwa halisi vijiko viwili, kahawa vijiko viwili na maji ya mchele kiasi kama hicho.

Wakati wa kuandaa unatakiwa kuchukua maji ya mchele uliochemka vizuri, kisha changanya kwenye maziwa yenye kahawa.

Ukimaliza unatakiwa kuchanganya vizuri mpaka iwe kati hali ya uji mzito, halafu paka usoni kwa kuzungusha mikono.

Ukimaliza, jipake usoni na uache kama dakika tatu ili ikauake vizuri. Ukihakikisha imekauka anza kujisugua usoni taratibu.

Mchanganyiko huu unatakiwa kuutumia kwa muda wa wiki mbili.

# MAPISHI

## Na Mary Geofrey


# Scones za maboga, nazi na maziwa



UNGA wa ngano kilogramu moja, hamira kijiko kimoja cha chakula, chumvi nusu kijiko cha chai, sukari kijiko kimoja kidogo cha chai, maziwa au tui bubu la nazi au vyote.

Uji mzito wa maboga ya njano yaliyochemshwa na kupoa kikombe kimoja cha chai. vanila nusu kijiko kidogo cha chai na siagi kidogo.





**NAMNA YA KUANDAA**

Andaa maji ya uvuguvugu ujazo wa nusu kikombe kidogo cha chai, weka hamira kwenye maji ya uvuguvugu kisha funika kwa muda wa dakika tatu hadi tano.

Andaa unga wa ngano, pasha moto sufuria ya kukandia, chemsha mafuta ya kula mililita 20 hadi 30 na umimine hamira kwenye unga.

Changanya vizuri kisha mimina mchanganyiko kwenye mafuta yanayochemka, koroga kwa kutumia mwiko.

Ongeza maziwa au tui la nazi na endelea kukanda hadi unga uwe laini na usigandane na sufuria, kisha weka siagi kidogo na endelea kukanda.

Weka vanila kisha endelea kukanda, paka sufuria mafuta, weka mchanganyiko wa unga uliokanda kisha funika na weka sehemu yenye uvuguvugu au joto kwa dakika 30 hadi 45 ili unga uumuke vizuri.

Ukishakanda tena gawa matonge madogo madogo, panga kwenye mduara wa sufuria ambayo umepaka mafuta na weka kwenye sehemu yenye joto au vuguvugu kati ya nyuzi 80°C hadi 120°C kwa muda dakika 45.

Unga ukishaumuka vizuri weka moto kwenye jiko la mkaa ili liwe la moto kwa dakika 10, punguza moto na injika sufuria yenye scones juu ya jiko.

Palia mkaa wenye jivu la moto juu ya mfuniko na subiri kwa dakika 10 kisha funua uangalie kama zimeiva.

Ukifunua na kuona zimebadilika rangi na kuwa kahawia (brown), zipake siagi kwa juu na funika. Baada ya dakika mbili mimina scones zako kwenye chombo kisafi na acha zipoe na zitakuwa tayari kwa mlo wako.



# Sakafu yako ya jana yaweza kuwa muujiza wa leo



KILA siku tunashuhudia mabadiliko ya maisha kutokana na utandawazi katika karne ya leo.

Mambo yaliyofanyika jana siyo yale yanayofanyika kesho wala keshokutwa, kila siku yanaibuliwa mapya au kwa mtindo mwingine au kwa ubora zaidi.

Leo tunaangalia ubora uliopo sasa katika uwekaji wa sakafu ndani ya nyumba.

Katika nyumba, sakafu ni miongoni mwa vitu vinavyochangia kupendezesha nyumba na hata pale inaposakafiwa kwa utaalamu mzuri.

Yapo baadhi ya mambo yanayopaswa kuzingatiwa kabla ya kusakafia nyumba ambayo Msanifu Majengo, David Kashozi, anayaeleza kuwa kabla ya kuweka sakafu, ni muhimu kuangalia rangi ya nyumba ili visipishane.

Jambo la pili linalopaswa kuzingatiwa wakati wa kufanya uchaguzi wa sakafu ni ubora wake.

Jambo la tatu ni kuchagua sakafu ambayo ni rafiki na salama kwa makundi yote ya watu wanaoishi katika nyumba.

"Chagua sakafu ambayo haitawakwaza baadhi ya watu kulingana na umri wao hususani watoto, wazee na wagonjwa, maana nyingine zina utelezi mkali," anasema Kashozi.

Jambo la nne, anasema ni vizuri kuzingatia kuchagua sakafu ambayo ni bora na inadumu kulingana na bajeti uliyojiwekea kabla ya kubadili nyingine.

"Japokuwa tunashauri kwamba usiwe nyuma ya wakati sana, hakikisha ni bora, lakini inaendana na wakati," anasema Kashozi.

Na jambo la tano, anashauri kwamba ni vyema kufanya maandalizi mapema ya aina ya sakafu unayoitaka.

MPANGILIO

## Dondoo wakati wa kusafisha sakafu ya marumaru

ONDOA vipande vya mawe au mchanga kwenye sakafu kwa kutumia fagio laini. Hakikisha ngazi na sehemu zilizoinuka hakuna uchafu utakaoangukia wakati unasafisha.

Ondoa mazulia na uhifadhi sehemu kavu, pia safisha kwanza kitanda na viti kabla hujaosha sakafu.

Fagia kwa uhakika sakafu kwa ufagio laini ili kuondoa umbi na aina nyingine ya uchafu.

Tumia fagio lenye tambi kwa ajili ya kusafishia sakafu, tumia maji yenye sabuni kabla ya kusafisha kwa maji safi. Kausha vizuri kwa kutumia kitambaa au kifaa maalum.




# KATUNIKA KI'DOMOKRASIA

**BY ABDUL KINGO - 2020**

SMS - 0621 412 879

## JUKWAANI



















***KINYUNYIZO CHA LEO...**

**... MTETEZI WA MWIZI ZIRAILI...**

MAKALA MAALUM

# Gamanywa: Magufuli chaguo sahihi kwa maslahi ya taifa



***HIVI karibuni Askofu Mkuu wa Wapo Mission International, Sylvester Gamanywa, alizindua kitabu kiitwacho 'Uzalendo na Falsafa ya Mamlaka' akihusisha uchaguzi mkuu wa Oktoba 28, mwaka huu. Ifuatayo ni sehemu ya mahojiano kuhusu Uzalendo na Mamlaka...***

SWALI: Wakati wa uzinduzi wa kitabu chako cha Uzalendo na Falsafa ya Mamlaka ulihutubia mkutano wa waandishi wa habari kwa kusema haiwezekani kumtenganisha Rais John Pombe na maslahi ya taifa. Ulikuwa na maana gani?

JIBU: Kabla ya kujibu swali hilo, naomba nitoe tafsiri sahihi kuhusu maslahi ya taifa. Neno masilahi ya taifa kwa ujumla linaloshikiliwa kuwa chombo huru tofauti na maslahi ya maeneo ya chini ama vikundi au mataifa mengine au vikundi vya kitaifa.

Maslahi ya nchi ni ardhi, rasilimali za asili kuanzia maji, mimea, wanyama, na madini. Mambo mengine ambayo ni maslahi ya taifa ni haki za kiraia kwa raia wote pasipo upendeleo wala ubaguzi kwa maslahi ya maeneo ya kikanda, au vikundi na mataifa mengine au vikundi vya kitaifa.

Hatuwezi kumtenganisha Rais na maslahi ya taifa kutokana na uwezo wake mkubwa aliouonyesha kwa kusimamia na kudhibiti usalama wa maslahi ya taifa pasipo kujali maslahi ya vikundi vya kisiasa, kidini na kimaeneo.

Maelezo ya kina kuhusu uzalendo na maslahi ya taifa nimevichambua ndani ya kitabu nilichokizindua cha Uzalendo na Falsafa ya Mamlaka. Kila atakayekisoma atajua ukweli wa mambo ulivyo.

**SWALI: Unataka jamii iamini kwamba watu wasipomchagua Rais Magufuli hawajali maslahi ya taifa?**

**JIBU**: Kuna kuwapo kwa maslahi ya Taifa na kuna kuwapo kwa mtu mwenye uwezo wa kusimamia na kudhibiti na kulinda maslahi ya taifa. Kutokuwepo kwa Rais Magufuli madarakani kunamtegemea Mwenyezi Mungu aliyemteua tangu mwaka 2015 na kumpa mamlaka aliyo nayo.

Hoja ninachotilia mkazo hapa ni jamii kupambanua mgombea wa urais kwa kigezo cha uwezo na uzoefu wa mgombea alionao katika kusimamia na kulinda maslahi ya taifa kwa manufaa ya raia wote.

Pamoja na kuwapo kwa wagombea wa vyama vyote wanaojinadi ili wachaguliwe kushika mamlaka ya nchi, kwa wakati huu kila Mtanzania ambaye ni mzalendo wa kweli, nina imani atapiga kura ya uzalendo kwa kumchagua kiongozi mwenye sifa na uwezo pamoja na uzoefu wa vitendo katika kusimamia na kulinda maslahi ya taifa.

**SWALI: Kwa maneno yako na mtazamo wako unatafsiriwa kwamba mwaka huu umejiingiza kwenye siasa moja kwa moja na umeacha kuhubiri injili. Unajiteteaje hapo?**

**JIBU:** Nimeshiriki uchaguzi kuanzia awamu ya tatu, awamu na ya nne. Ni kila awamu niliandika kitabu chake kama nilivyofanya mwaka huu. Hata hivyo, swali lako linatoa mtazamo kwamba mtumishi wa Mungu kujiingiza kwenye siasa ni kuiacha imani na kuacha utumishi wa Kristo.

Huu ndio mtazamo potofu ambao shetani ameutumia miaka yote kuwafanya watumishi wa injili wakae kimya na kuchagua kutokuwa na upande wowote hata katika mambo yenye kuathiri maadili ya kiimani na kuharibu maslahi ya Taifa.

Majuzi tumetembelewa na Rais wa Malawi, Lazarus Chakwera, Askofu mkuu mstaafu wa Kanisa la Assemblies of God Malawi. Leo ni Rais wa Malawi, je, amerudi nyuma kiroho? Ameiacha injili ya Kristo kwa kuingia katika siasa? Je, hatusomi katika maandiko kwamba wafalme wa nchi huwekwa na Mungu mwenyewe na wametajwa kuwa nao watumishi wa Mungu?

Ninapohimiza jamii kupiga kura za uzalendo na si kura za usaliti, hii ni huduma ya kichungaji kwa jamii. Hii ndiyo kazi ninayoifanya kwa sasa kwa majira haya. Nawanusuru kondoo wa kijamii kulinda uraia mwema kwa kuepukana na wagombea wa washabiki wa kisiasa ambao wamepania kubadilisha sheria za maadili mema ili kuifanya nchi ya mashoga.

**SWALI: Huamini kwamba kambi ya upinzani nayo pia inajali maslahi ya taifa ndiyo maana ilani za vyama vyao zimeahidi kuwaletea maendeleo ya watu moja kwa moja badala ya maendeleo ya vitu tu?**

**JIBU:** Hapa si suala la mimi kuamini au kutokuamini. Ni suala la kuzitathmini ilani za vyama kwa kigezo cha maslahi ya taifa yasiyohusisha viashiria vya kubomoa misingi ya utaifa wetu na kuturudisha kwenye maslahi ya vikundi na maeneo ya kikanda ambapo Tanzania tulikwisha kuvuka viwango vya ubaguzi wa kimaeneo na kimakundi katika jamii

Kinachotisha zaidi ni dhana za baadhi ya wagombea wanaotangaza hadharani kwamba wakipewa kuongoza nchi, wataweka rehani rasilimali za nchi kwa ajili ya kupata mikopo kutoka kwa matajiri wa nje, wakifikiri hii ndiyo njia ya kuwaletea wananchi maendeleo ya moja kwa moja. Kwa lugha nyingine wakipewa nchi hatua ya kwanza ni kuuza nchi kwa mabeberu.

**SWALI: Tufafanulie kwa kina ni nini maana sahihi ya maneno haya uzalendo na usaliti na dhana hii umeitoa wapi?**

**JIBU:** Kwanza suala la uzalendo na usaliti si dhana kama unavyoitafsiri wewe. Mimi ninaongelea uhalisia wa mazingira ya kisiasa yaliyoghubika kampeni za uchaguzi mkuu mwaka huu. Tangu mwanzo nilipotaja maneno haya ya usaliti na uzalendo nilikwisha kuona wazi kwamba ushindani wa kisiasa uliopo hivi sasa si wa ushawishi wa ubora wa ilani zenye kusimamia na kulinda maslahi ya taifa, bali ni maneno ya chuki, shutuma, tuhuma, na hisia zilizojaa hasira na vinyongo.

Pia kuna upande mwingine wa kizalendo ambao unakiri na kupongeza juhudi za maendeleo ya kiuchumi yaliyofanyika chini ya awamu ya tano na wenye kuhamasisha wapigakura kupiga kura za uzalendo kwa ajili ya kumchagua kiongozi mwenye uwezo na uzoefu wa kulinda maslahi ya taifa kwa manufaa ya raia wote.

Uzalendo ni hali ya mtu kuwa tayari kuifia nchi yake. Mzalendo ni mtu anayedhihirisha kuwa anaipenda nchi yake na yuko tayari kuitetea na kuifanyia mema yote hata kuifia. Mzalendo wa kweli ni mtu ambaye anapenda sana na yuko tayari wakati wote kuiendeleza na kuitetea nchi yake, viongozi, mipango yake na watu wake.

Uzalendo pia unahusu utayari wa kila raia kulinda uhuru wa nchi na mipaka yake, amani na utulivu kwa raia , pamoja na kuwa tayari kulinda rasilimali za nchi kwa maslahi ya raia wote. Uzalendo huambatana na tabia ya kutii na kuheshimu utawala na Mamlaka za nchi.

Usaliti ni tendo la kutoa siri za mtu, kikundi, au nchi kwa adui wa mtu, kikundi au nchi. Mwenye kutenda usaliti huitwa msaliti. Msaliti ni mtu anayemsaidia adui wa mtu au taifa kwa kumpa taarifa za siri zitakazotumika kusababisha madhara kwa msalitiwa. Msaliti ni mtu yeyote anayekabidhi au kuficha siri au taarifa za usalama wa mtu au nchi kwa hila pasipo kujulikana kwa msalitiwa.

Usaliti dhidi ya nchi ni kitendo cha mtu au raia wa nchi kutoa ama kwa siri au hadharani, taarifa kwa nia ya kuichongea nchi ionekane vibaya kwa watu wa nchi nyingine au katika anga za kimataifa.

Katika miaka ya hivi karibuni, tumeshuhudia baadhi ya Watanzania wenye amana ya uongozi wa nchi kwa kupitia vyombo vya habari vya kimataifa wakisema taarifa hasi kwa nia ya kuichonganisha Tanzania ionekane vibaya kwa watu wa mataifa mengine hususan anga za kimataifa. Huu ndio usaliti mkubwa dhidi ya nchi.

Ni Tanzania peke yake duniani nchi ambayo imejaliwa hekima ya kuchukuliana na wasaliti wa aina hii kiasi hata cha kuwapa fursa ya kugombea tena nafasi za uongozi wa nchi.

**SWALI: Unataka jamii iamini kwamba kambi ya upinzani ndio wasaliti na chama tawala ndio wazalendo?**

**JIBU: Suala la usaliti ni mtambuka. Liko vyama vyote kuanzia chama tawala na upinzani, na hata kwa wasiokuwa na vyama kabisa.**

**SWALI: Mpigakura atajuaje kwamba kura anayokwenda kupiga ni ya uzalendo na si kura ya usaliti?**

**JIBU:** Swali zuri sana. Mpigakura ambaye moyoni mwake anamfahamu kwa uhakika mgombea wa urais ambaye ana sifa na uzoefu wa kusimamia na kulinda maslahi ya nchi, na kwa sifa hizo akajipanga kwenda kumpigia kura, ajitambue kwamba anakwenda kupiga kura ya uzalendo.

Na mpigakura yeyote ambaye anamfahamu mgombea mwenye sifa na uzoefu wa kulinda maslahi ya taifa, lakini kwa sababu za chuki binafsi dhidi ya mgombea huyo na akampigia kura mgombea mwingine ambaye hana sifa wala uzoefu wa kulinda maslahi ya taifa, basi ajitambue kwamba anakwenda kupiga kura ya usaliti dhidi ya nchi yake.

**SWALI: Una uhakika gani kwamba Rais Magufuli atashinda kwenye uchaguzi mkuu mwaka huu na kwa ushahidi gani wa kitafiti?**

**JIBU:** Uhakika wa ushindi wa Rais Magufuli hautokani na ushabiki binafsi wa kisiasa. Nina uhakika kutokana utafiti wa kimataifa uliofanyika kuhusu mwenendo wa kampeni za uchaguzi unaoendelea nchi Tanzania. Sababu kubwa zilizotolewa za walio wengi kumchagua Rais Magufuli zilikuwa uwezo wa kulinda maslahi ya taifa na uadilifu.

SAFU

# ‘Simba Luwala’ na mabasi yaliyotikisa



Na Adam Fungamwango

SIFIKIRII kama kuna mtu aliyeishi au kutembelea Dar es Salaam katikati ya miaka ya 1980 hadi 1990 na kwa sasa anaishi sehemu yoyote ile duniani, achilia mbali Tanzania, haifahamu daladala maarufu iliyokuwa inaitwa ‘Simba Luwala.’

Basi hili lilifanya safari zake kati ya Mwananyamala na Kariakoo. Wakati haliko kwenye safari, lilionekana sana kupaki maeneo ya Fire jijini Dar es Salaam kwenye gereji moja hivi.

Sifa ya daladala hii ya kwanza kabisa ni kujaza abiria wengi hadi wengine walikuwa wakining’inia. Lakini pia ilionekana haikuwa madhubuti sana, yaani spana mkononi. Watoto wa mjini sasa wanasema ‘tripu moja shamba, tripu moja gereji.’ Wakati huo mtu akisemwa kwa ubaya, au kwa ubovu, basi atafananishwa na daladala hilo.

Hata tuliokuwa tunakimbia mchakamchaka shuleni wakati huo, tunaimba nyimbo za shule, lakini tukiwa mbali na shule kuna aina fulani ya nyimbo zetu za kutunga wenyewe na moja kati ya wimbo huo ni kuimba daladala hiyo.

“Daladala Simba Luwala Daladala Simba Luwala, juu zege, chini makaratasi.” Ni wimbo ambao ulikuwa unaonyesha jinsi gani lilionekana mbele ya jamii wakati huo.

Lakini ukweli unabaki pale pale kuwa ndiyo daladala iliyokuwa mkombozi wa wakazi wa Mwananyamala wakati huo barabara ilikuwa mbovu sana. Daladala nyingi ziligoma kabisa kufika Mwananyamala na ziliishia Kinondoni tu. Simba Luwala, pamoja na uspana mkononi wake, ilifika na kumudu vikwazo vyote vya ubovu wa barabara.

Ilikuwa na rangi nyeupe na nyekundu, ikipambwa na picha ya simba wawili ubavuni wakiwa wanaruka, lakini wakiangaliana, mmoja mbele kidogo ya basi na mwingine nyuma.

Vyovyote itakavyosema au kuandikwa, lakini ‘Simba Luwala’ inabaki kuwa ndilo basi au daladala maarufu kabisa jijini Dar es Salaam kuwahi kutokea kwenye historia ya magari hayo nchini tangu yalipoanza kuruhusiwa kuchukua abiria.

Awali, ni Shirika la Usafiri Dar es Salaam (UDA) ambalo liliruhusiwa kubeba abiria jijini lakini ilifika wakati lilizidiwa na ndipo mwanzoni mwa miaka ya 1980, aliyekuwa Waziri Mkuu wakati huo, Edward Moringe Sokoine (sasa marehemu), akaruhusu mabasi ya watu binafsi kusafirisha abiria na wakati huo, yalianza kwa kutoza nauli ya Sh. tano, fedha hiyo ikiitwa dala. Hapo ndipo jina la daladala lilipopatikana.

‘Simba Luwala’ likiwa moja ya mabasi ya mwanzo kubeba abiria Dar es Salaam.

Mengine ni ‘Chako Changu’, ‘Again’, ‘Najimunisa’, na moja basi zuri kabisa aina ya Coaster wakati huo zikiitwa ‘vi-luxury’ ndiyo zilikuwa zikiingia ilitwa ‘Scaba Scuba’ au ‘Scaba Line’.

Kule Mwenge Kariakoo kulikuwa na daladala zilioitwa ‘Makadidi’ na ‘Kiabakari’

Kutoka Temeke hadi Posta kulikuwa na daladala maarufu ya ‘Tim Yulee’ inayosadikiwa kuwa ndiyo ilikuwa daladala la kwanza kuwa na redio kaseti.

Dalala zingine maarufu zilikuwa ‘Dau la Mnyonge’, iliyoonekana kuwa na hili lilionekana kama lina undugu hivi au ni la mmiliki mmoja na ‘Simba Luwala’, kwani nalo lilionekana maeneo ya Fire yakiwa pamoja wakati hayabebi abiria, ‘Dunia Hadaa’, ‘Ruziki kwa Mungu’ haya yalionekana kutoka Tandika au Temeke kwenda Posta, lakini pia kulikuwa na daladala lingine maarufu ‘Famagusta Saratoga.’

Maeneo ya Uwanja wa Ndege hadi Posta kulikuwa na daladala la ‘Wanajikata’, Pugu Kariakioo ilikuwapo ‘Sea Never Dry’, ‘Masumin’ au ‘Jaribu Tena’, ‘Inter Programmes’, ‘Scolastica’, na ‘Jadide’.

Maeneo ya Kurasini, Shimo la Udongo kwenda Kariakoo kulikuwa na dalada lililoitwa ‘Kitmeer’, halafu kuna ‘Jai Sanka’, na ‘vi-luxuary’, Kabombe Tours lililokuwa kilienda Muhimbili kutoka Kariakoo, na ‘Beach Boys’ kutoka Buruguni hadi Posta.

Pia kuna daladala inaitwa ‘Wifi Naye’ kutoka Mwananyamala -Stesheni ambayo awali ilikuwa inatoka Lindi hadi Dar, lakini baada ya kuchakaa ikafanywa daladala.

Tukija kwenye mabasi ya aina ya Coaster au ‘luxury’ kutoka Dar kwenda Moro kulikuwa na ‘Mudy Punk’ na ‘Chisu Papino’, ‘Pwani Tours’ ‘Tuvuke’ (Kariakoo- Mlanizi),

Kwa mabasi ya mikoani kulikuwa na ‘Moro Best’, ‘Dar Oye’ ‘Comfort’, ‘Siri Yako’, ‘Kipengule’ na mengine, huku ‘Jogoo la Shamba’, ‘Mfamao’, ‘Mwinyihija’ yalikuwa yakitoka Dar, Lindi na Mtwara.

Kutoka Dar, kwenda Mbeya Kyela kulikuwa na mabasi ‘Lea Watoto’, ‘Huduma’, Ntahena’, ‘Upendo’, ‘Karanja’, ‘Obamka’, ‘Wema’, Mpegwa’.

Bado watu yanayakumbuka mabasi ya ‘Nyuki’, ‘Mzalendo’, ‘Dunia Muzima’, ‘Kiswele’, ‘Super Champion, ‘Njuweni’, ‘Masama Cliff’, ‘Masama Safari’, ‘Yarabi Salama’ na Yarabi Toba’, na ‘Embakassy’.

Wakati wa Dodoma wao walikuwa na mabasi ya ‘Dodoma Wadeka’, ‘Deluxe Coach’, ‘Super Star’, ‘Metro Coach,’

na ‘The Big Mayai’.

Bado pia huwezi kuyasahau mabasi ya’Air Msae’, ‘Victoria Tours’, ‘Mkuu Trans’, ‘Bembea’, ‘Taqwa’, ‘Takrim’, ‘Shengena’, ‘Kwacha’, ‘Ngorika’, ‘TTBS’, ‘Born City’, ‘Tawaqal’, ‘Zainab’, ‘Widambe’, ‘Upete’ ‘Wifi Naye’, ‘Mwafrika’, ‘Fresh ya Shamba, KIDECO,’Kwamwanga Line’, ‘Mweleko’, ‘Katarimos’

# Wanasiasa baada ya madaraka mmejiandaa!

Na Magabilo Masambu



MIEZI miwili tu baada ya kupitishwa kwa Azimio la Arusha katika kikao cha Halmashauri kuu ya TANU mwishoni mwa Januari 1967, Mzee Kawawa aliwatangazia wabunge kwamba kama wana maswali juu ya Azimio wayawasilishe na yatajibiwa. Katika kuitikia wito huo wabunge waliwasilisha takribani maswali 21 ambayo yalijibiwa na Mwalimu Nyerere mwenyewe. (Azimio la Arusha Maswali na Majibu, 2017, Prof. Issa Shivji).

Katika maswali 21yaliyotolewa na wabunge, swali ambalo Mwalimu alidai lilikuwa swali chafu kupita maswali yote na lililoulizwa zaidi na viongozi wengi ni hili “Hali ya mwanasiasa haina uhakika. Leo ni waziri kesho si waziri; leo ni mbunge baada ya miaka mitano si mbunge; leo ni katibu wa mkoa au wilaya kesho katupwa na wananchi kwenye uchaguzi je, Azimio la Arusha haliwaonei viongozi hawa ikiwa litawazuia kutumia njia zingine kujitengenezea maisha yao ya baadaye?

Baadhi ya miiko ya uongozi iliyoelezwa katika Azimio la Arusha uk 38 ni pamoja na kiongozi kutoruhusiwa kumiliki hisa katika kampuni yoyote, kutokuwa na mishahara miwili au zaidi, kutokuwa na nyumba ya kupangisha nakadhalika, viongozi wakahoji je, huko siyo kuwafanya viongozi baada ya madaraka kuishi maisha ya tabu?

Pamoja na mambo mengine Mwalimu anahoji “Ni kiongozi gani ambaye wakati wa uchaguzi anawaambia wananchi wamchaguwe ili ajitengenezee hali yake ya baadaye? Ni nani ambaye alipata kazi katika TANU awe Katibu wa wilaya au mkoa kwa lengo la kutengeneza maisha baada ya uongozi wake? Kila tunapotaka kazi ya kisiasa japo ni ya kuchaguliwa kwa kura au kuteuliwa, husema tunaitaka kazi hiyo ili tuweze kuwatumikia watu, kulinda haki zao na kuwasaidia kutimiza mahitaji yao. Kiongozi ana haki gani basi mara tu baada ya kuipata nafasi hiyo kusema anataka kuitumia ili kujitengeneza maisha yake ya baadaye? Vipi kuhusu wananchi ambao maisha yao yote wanaishi bila nafasi za kisiasa wao wanaendeshaje maisha yao?

Kuelekea uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba hii 28, 2020 ni vizuri tukatafakari kwa pamoja kwamba Je, tunakwenda kuchagua viongozi ambao wanaomba nafasi ili wakatengeneze maisha yao ya baadaye au tunachagua viongozi tutakaoshirikiana nao kuhakikisha tunajiletea maendeleo yetu wenyewe? Je, ni kweli kwamba hofu ya maisha baada ya madaraka ni sababu mojawapo yenye kuwafanya viongozi kuwa wabadhirifu wa mali za umma ili kutengeneza maisha yao ya baadaye? Lakini tunafahamu baadhi ya ngazi mbalimbali za uongozi kama udiwani, ubunge na urais una kiinua mgongo (mafao) baada ya madaraka, lakini pia wakati wa kazi kuna mishahara kwanini viongozi wasitumie hicho kutengeneza maisha yao ya baadaye badala yake mpaka wafanye unadhirifu wa mali za umma?

Nguvu nyingi zinazotumika kwenye uchaguzi zinaweza kuthibitisha bila shaka kwamba inawezekana kweli viongozi wengi wanayataka madaraka ili kutengeneza maisha yao binafsi pamoja na kwamba hakuna anayesema juu ya hilo badala yake kinachozungumzwa sasa ni juu ya kuwatumikia wananchi na ingependeza zaidi haya yanaosemwa juu ya watu (wapiga kura) yawe ya kweli pindi washindapo nafasi za uongozi kinyume chake itakuwa ni utapeli.

Hofu ya nini? Kama ulikuwa mkulima kabla ya kuwa kiongozi unapokuwa kiongozi unapata mshahara kwa kazi hiyo maana yake utakiboresha kilimo chako na kuwa cha kisasa, tabu ya viongozi wetu wengi ni kujiona kwamba uongozi ni daraja lingine kabisa na kwamba ukishakuwa kiongozi kurudi kufanya shughuli za kawaida ni kujidhalilisha si kweli hata kidogo. Mtazamo huu ndiyo unawafanya viongozi wengi wawe mbali sana na wananchi kwa kudhani kwamba wao sio watu wa kawaida tena kwa kuwa sasa wanaitwa waheshimiwa na hivyo kuwafanya wananchi wawaogope hata kuwaeleza matatizo yao.

Uongozi sio sehemu ya kujitajirishia kama ulivyo mtazamo wa wengi bali ni daraja la kuwaunganisha watu pamoja na kuwatumikia, kiongozi anapaswa kuwa mtumwa sio bwana mkubwa, kwasababu kwa mujibu wa Katiba yetu ya nchi mamlaka yote hutoka kwa wananchi ndiyo waajiri.Tujitokeze Oktoba tuwachaguwe viongozi kwa manufaa ya umma.

***0689157789***
***magabilomjalifu@gmail.com***

# HADITHI

WASWAHILI wanasema mshika mawili moja humponyoka na karamu mbili zilimshinda fisi. Cecilia, msichana mwenye kila sifa ya kuitwa msichana mrembo, anaangukia kwenye mapenzi ya vijana wawili. Kati ya vijana hao, mmoja ni fukara na mwingine mwenye uwezo. Kutokana na mwenyewe kutokuwa na msimamo, anawaingiza vijana hao kwenye chuki na visasi, vilivyoambatana na wivu uliopindukia na kusababisha maafa makubwa. Ni kisa cha kusikitisha, kutisha na kuhuzunisha, lakini chenye elimu kubwa.

# Adui Namba Moja-3

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

WALIONGEA hili na lile. Wakabadilishana namba za simu. Kila mmoja akawa na ya mwenzie. Kwa siku mbili mfululizo hawakupigiana simu. Siyo kwamba kila mmoja alimsahau mwenzake.

Ukweli ni kwamba baada ya kuachana. Mashaka akili yake ikahamia kabisa kwa msichana yule. Aliona huenda ndiye akawa msichana sahihi aliyekuwa akimhitaji. Alikuwa na kila sifa za kuitwa msichana mrembo. Baadaye pia awe mke wa mtu.

Hakutaka kumpigia haraka haraka kwa sababu mbili. Kwanza isije ikaonekana kama amekufa na kuoza zaidi. Pili hakutaka kuonekana ni mtu mwenye tabia ya kupendapenda wasichana. Siku moja tu kupata simu yake tayari unaanza kumsumbua.

Siku ya tatu alimpigia simu. Wakaongea mengi na kuahidiana kukutana baada ya siku nne. Na kweli walikutana maeneo ya Magomeni Usalama.

Maongezi yalianza. Yaliishia kwa kuwa wapenzi. Ni kawaida tu kwa mwanamume na mwanamke wanapokutana mara ya kwanza hadi kuwa wapenzi au mtu na mke.

Mwanamume anaweza kukutana na mwanamke akaitwa baba, baadaye mjomba, halafu shemeji, siku nyingine kaka, tena na shikamoo juu. Mwisho wa siku akaitwa mpenzi, 'baby', na majina yote ya mapenzi, inawezekana kabisa baadaye akawa mume.

Mwanamke naye ni hivyo hivyo, anaweza akaitwa mama mdogo, kesho shangazi, dada, mwishoni akawa ndiyo mpenzi, au mke.


Hivi ndivyo ilivyokuwa pia ni Mashaka na Cecilia. Mapenzi yakanoga. Wakapendana haswa. Kila mmoja alijua anapendwa na mwenzake. Pamoja na hayo walikuwa bado hawajatambulishana kwa wazazi. Walikuwa wanajiandaa kufanya hivyo.

Aliyekuwa anajua mapenzi hayo ni Badaka. Mdogo wa Cecy ambaye alikuwa akifuatana naye wakati mwingine kwenda kwa Mashaka. Ndugu wachache na majirani ya Mashaka pia walilijua penzi hilo.

"Sasa limekwenda wapi?" Alijiuliza. "Cecy mpenzi wangu umekula nini?" Machozi yalizidi kumtoka. Dakika chache baadaye usingizi ukampitia, kabla ya kuamshwa na mlio wa simu na alipoiangalia jina lilikuwa la Cecy.

"Haloo." Aliwahi kuita.

"Unanisikia vizuri we kinyago?" Ilikuwa sauti iliyotokea upande wa pili. Ilikuwa sauti aliyoizoea. Ile ile ambayo zamani ilikuwa inambembeleza, kumliwaza na kumpa faraja.




**Ilikuwa rahisi kwa mwanamume kupishana naye akashindwa kugeuka. Iwe akikutana naye kwa mbele na lazima atageuka akishapitana naye, na hata kama atakuwa nyuma yake, akishampita tu atagauka kuangalia sura.**

"Baby imeamkaje?. Umeshindaje mpenzi? Umekula? Umelala? Nakupenda sana."

Hakujibu kitu. Alibaki anasikiliza nini kitazungumzwa. Lakini hakuna alichotegemea zaidi ya maneno ya 'shombo', shari na kukatisha tamaa.

"Nachokwambia ni hivi, kuanzia leo ukome kunifuatilia. Mimi si mpenzi wako tena, futa hilo wazo kwenye kichwa chako na kuanzia sasa tukimaliza hapa mimi nafuta namba zako, na wewe futa zangu."

Sauti hiyo haikuwa na mzaha. Haikuwa laini kama ile aliyoizoea. Ilikuwa ya kike lakini iliyokaza sauti, iliongea na msisitizo uliochanganyikana na dharau, na hasira kwa wakati mmoja.

"Hivi Cecy, unaweza kuniambia tatizo lililokufanya mimi unibadilikie ghafla kiasi hicho ni nini?" Sauti ya Mashaka ilionyesha kubembeleza.

"Hivi, kwani wewe hujui kukataliwa? Kwani kukataliwa kuna sababu. Nilipokupenda kulikuwa na sababu? Kama nilivyokupenda, ndiyo hivyo hivyo ninavyokukataa."

Mashaka hakujua sasa aseme nini. Midomo ilimcheza kwa hasira, huzuni na sononeko kwa wakati mmoja. Alihisi kizunguzungu. Nusura simu imdondoke, kwani mikono yake pia ilikuwa ikitetemeka.

Moyo wake ni kama ulidungwa sindano ya moto. Anampenda sana Cecy, lakini leo haelewi ni kitu gani kimembadilisha. Anatambua kabla ya hapo Cecy alikuwa anampenda.

Hata kama alikuwa hana kitu, msichana huyo alikuja nyumbani kwake akiwa na mchele, unga, samaki, nyama, mboga za majani akivifungasha kutoka kwao Kinondoni hadi Ubungo Maziwa. Mtoto wa kike anaingia jikoni na kupika, mchana wanakula, kingine kinabaki cha usiku, akiondoka kwenda kwao anamuachia mwenzake msosi.

Mawazo ya mwanzo wa penzi lao lilivyonoga, kuchanganya na alivyochoka na kunyong'onyea akiona jinsi penzi linavyoanza kufutika, usingizi mzito ulimpitia akiwa kwenye kochi

*****************************

Kwa sasa barabara ya Bagamoyo hasa maeneo ya Morocco hadi Mwenge kuna ujenzi wa barabara. Hii inasababisha wakati mwingine watembea kwa miguu wapite kando kabisa ya barabara ambapo wanatengenishwa na kamba zilizofungwa kwenye mapipa, ili kutenganisha magari na wapita njia.

Ilikuwa maeneo ya Makumbusho. Mmoja kati ya watembea kwa miguu alikuwa msichana mmoja mrembo.

Alikuwa si mrefu wala mfupi. Alikuwa maji ya kunde, mwenye ngozi nyororo. Alikuwa mwembamba kwa wajihi, lakini akiwa na kiuno kilichokatika na kuweka umbile namba nane.

Ilikuwa rahisi kwa mwanamume kupishana naye akashindwa kugeuka. Iwe akikutana naye kwa mbele na lazima atageuka akishapitana naye, na hata kama atakuwa nyuma yake, akishampita tu atagauka kuangalia sura.

Ilikuwa majira ya saa 7:00 mchana, wakati gari aina ya Toyota Corolla Rumion lenye rangi nyekundu likitokea maeneo ya Mwenge kwenda Morocco ilikuwa likitembea taratibu. Ilimpita msichana huyo na kwenda kupaki kwenye kituo cha Makumbusho kile cha nje kwenye mabasi yaendayo Kariakoo, Gerezani na Stesheni ambapo kinapakana na Makumbusho ya Taifa. Kwa sasa huwa hakina abiria wengi sana kwa sababu wengi huingia kwenye kituo cha ndani.

"Dada habari yako." Ni sauti iliyosikika ikitoka ndani ya gari ikimsalimia msichana yule baada ya kufika. Msichana alimwangalia anayesalimia na akawa kama hataki kujibu hivi.

"Dada nimesimamisha gari kwa ajili yako nikusogeze, nimekupita hapo nyuma kidogo nikaona nikusubiri nikusogeze, jua kali hili."

"Ahsante nashukuru." Sauti ya msichana ilisikika, lakini alionekana hataki kupanda na kulipita gari hatua 10 mbele.

Aliyekuwa akiendesha gari lile, alilisogeza tena mbele na alipofika alipo msichana kwa mara nyingine alisimama. "Dada twende nikusaidie lifti."

Lengo la msichana yule ilikuwa ni kuvuka barabara aingie kwenye kituo cha ndani ya Makumbusho kupanda daladala ya kwenda Kinondoni.

Alikuwa amechoka kutokana na jua kali. Kweli alihitaji lifti, lakini hakutaka kujionyesha kuwa ana shida kiasi kile.

"Kwani wewe unaenda wapi kaka?" Kwa mara ya kwanza sauti ya msichana ilisikika.

"Naenda Kariakoo, wewe unaenda wapi?"

"Kinondoni."

"Basi nitakupitisha tu pale, njia si hiyo hiyo?"

Msichana alilegeza msimamo. Akafungua mlango akapanda.

"Unaitwa nani?" Aliuliza dereva wa gari lile.

"Jina langu Cecilia."

"Okay jina zuri, mimi naitwa Zahir."

"Nashukuru kukufahamu."

Hivi ndivyo walivyokutana Zahir na Cecilia. Walipeana namba za simu. Walianza kuwasiliana.

Zahir alionyesha kumhitaji Cecilia. Haikuwa ajabu, kwa sababu hakuna msichana yoyote mrembo asipendwe na wanaume tofauti.

Kilichogomba hapo ni msimamo wa Cecy mwenyewe. Kutakiwa jambo moja, kukubali au kukataa ni jambo lingine.

Cecy alijua kuwa ana mpenzi aitwaye Mashaka, lakini hakuonekana kuwa na msimamo.

Awali alisita. Lakini zawadi za magauni, blauzi, vipedo, vitenge, pesa vilimlainisha moyo.

Taratibu alianza kumsaliti Mashaka. Akawa na wapenzi wawili kwa wakati mmoja.

Siku zote penzi haligawanyiki. Haiwezekani ukawa na mpenzi zaidi ya mmoja, likaganyika nusu kwa nusu.

Hata ukiwa na wake wanne, ni lazima penzi litaelemea kwa mmoja zaidi.

Wazee wa zamani walisema dunia, mali na shamba vyote vinagawanyika, lakini siyo penzi. Lenyewe litafanya kila njia, upande mmoja litazidi.

Ndivyo ilivyokuwa. Kutokana na kupofushwa na uwezo wa kipesa wa Zahir, penzi likaelemea zaidi kwake kuliko kwa Mashaka.

Na kibaya zaidi aliona kama vile anamletea kiwingu, hivyo alitaka kuwa huru na mpenzi wake Zahir. Watanue. Waende popote pale bila kuhofia chochote wala vikwazo. Hivyo ndivyo Cecy alipoamua kumtema Mashaka.

**INAENDELEA JUMAPILI**



# KAYUMBA AMKANA UWOYA

MWANAMUZIKI wa BongoFleva, Kayumba Asosie, amewalaumu watu wanaoshinda kwenye mitandao ya kijamii kwa kuharibu urafiki wake na msanii wa filamu, Irene Uwoya.

Kayumba kupitia EATV, amesema yeye na Irene walikuwa marafiki wa kawaida, lakini baada ya kuzuka maneno waliamua wote kukaa pembeni kuepusha shari.

"Irene Uwoya alikuwa mshikaji wangu na tukaishia kwenye ushikaji, walivyoanza maneno yao tukaona bora tutulie tusiendelee maana ana familia yake na ana mtoto mkubwa, watu wa mitandaoni wanafiki sana sijawahi kukutwa na taulo nyumbani kwake japokuwa nilikuwa naenda sana, halafu mbona ana watu wengi kwanini naonekana mimi tu" amesema

## Harmorapa ajigamba hakuna mwingine

RAPA ambaye alikuja kwa kasi, kisha kuzimika kama mshumaa, Harmorapa, amejigamba kwamba cheni zake anazovaa zina thamani ya dola 10,000 sawa na Sh. milioni 23.

Akizungumza kwenye shoo ya Friday Night Live ya East Africa TV, msanii huyo ambaye kwa sasa ana muonekano mpya, amesema kuvaa urembo huo si kwamba amerudi kwenye ukoloni, bali ni vitu anavyovipenda na vyenye gharama kubwa.

"Hii cheni mimi mwenyewe hata sielewi nimejikuta tu inatokea, ukisema nimerudi ukoloni hapana wala sikuwepo kipindi cha ukoloni kwanza enzi za ukoloni sijakuwepo, thamani yake ni dola 10,000 japo siipendagi kwa sababu watu hawawezi kuamini



## Queen Darleen ajifungua mtoto wa kike

HATIMAYE msanii wa muziki wa kizazi kipya, Queen Darleen na mume wake, Isihack, wamepata mtoto wao wa kwanza.

Kupitia ukurasa wa wanandoa hao, jana asubuhi waliposti picha ya mtoto huyo wa kike ambaye wamempa jina la Balqis.

Hata hivyo, sura ya mtoto huyo ilifichwa, huku wakiambatanisha ujumbe wa kumshukuru Mungu kwa kumpatia zawadi hiyo.



HABARI MICHEZO

# Ancelotti, Calvert-Lewin watwaa tuzo ya mwezi

**LONDON,** England

KOCHA Mkuu wa Everton, Carlo Ancelotti, ameteuliwa kuwa kocha bora wa Septemba kwenye Ligi Kuu England.

Ancelotti amekuwa na mwanzo mzuri kwenye ligi hiyo kwa kushinda mechi zake zote za mwanzo za msimu huu.

Licha ya mwanzo mzuri, kocha huyo mwenye historia kubwa barani Ulaya alishindwa kufanya vizuri alipochukua timu kwa mara ya kwanza msimu uliopita kutoka kwa Marco Silva ambapo alikiongoza kikosi hicho kumaliza nafasi ya 12 kwenye msimamo.

Msimu huu baada ya kufanya usajili mzuri, ameshashuhudia timu yake ikiondoka na alama 12 katika mechi nne za mwanzo na klabu hiyo inakamata nafasi ya kwanza.

Kutokana na kuwa kwenye ubora, amefanikiwa kuwapiku makocha wengine na kushinda tuzo ya kocha bora wa Septemba na kuwa kocha wa kwanza kushinda tuzo hiyo msimu huu.

Mbali na kocha huyo, straika wake katika klabu hiyo ya Everton, Calvert-Lewin ameshinda tuzo ya mchezaji bora wa mwezi.



# SUAREZ AELEZEA ALIVYOLIA BARCELONA




**MADRID,** Hispania

LUIS Suarez ameelezea kumaliza wakati mgumu aliokutana nao pale Barcelona na sasa ameanza maisha mapya kule Atletico Madrid lakini amesikitika kumwacha nyuma, Lionel Messi pale Camp Nou.

Straika huyo wa kimataifa wa Uruguay hakuwa kwenye mipango ya kocha mpya, Ronald Koeman, akiwa amefunga mabao 198 katika misimu sita iliyopita.

Wakati Suarez aliambiwa na Barcelona hahitajiki tena, mchezaji mwenzake na nahodha, Messi alikuwa akitaka kuondoka, huku Manchester City wakionekana kumnyatia.

Akizungumza baada ya Uruguay kupata ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Chile kwenye mashindano ya kufuzu kombe la Dunia, ambapo yeye alifunga bao lake la 60 kwa nchini yake, Suarez ameelezea namna wote wawili, yeye na Messi walivyokabiliwa na wakati mgumu.

"Sikushangazwa kuhusu Messi kwa sababu namjua vizuri, nilijua maumivu aliyonayo," alisema Suarez.

"Alihisi wamenifukuza mimi klabuni. Kulikua na njia nyingine yakufanya mambo kwa usahihi na mimi.

"Ilikuwa miaka sita mirefu ambayo ilimuumiza pia yeye. Nilimwona kama rafiki na najua namna gani alivyokuwa anaumia kwenye nafasi yake.

"Nililia kwa kile nilichokuwa napitia, lakini sasa nipo na maisha mapya hapa Atletico Madrid."

Suarez kabla ya kutua Barcelona alicheza pia kule Ajax na baadaye Liverpool.

# *Eriksen akerwa kukaa benchi Inter*

**MILAN,** Italia

KIUNGO wa Inter Milan, Christian Eriksen, amesisitiza hataki kukaa benchi kwa msimu wote baada ya kuelezea kukatishwa kwake tamaa.

Eriksen aliondoka Tottenham kwenda kujiunga na Inter Januari mwaka huu, lakini raia huyo wa Denmark ameshindwa kujiimarisha yeye mwenyewe ili kupata nafasi kwenye kikosi cha kwanza cha Antonio Conte.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 amecheza dakika 73 tu kwenye Serie A msimu huu, akiwa ameanza katika mechi nane kati ya 17 za Ligi Kuu Italia msimu wa 2019-20.

Kwa ujumla, Eriksen ameanza katika mechi 11 kwenye mashindano yote msimu uliopita pale Inter.

Alipoulizwa kuhusu hali hiyo wakati akiwa na kikosi cha Denmark kinachoshuka dimbani leo Jumapili kucheza dhidi ya Iceland kwenye Ligi ya Mataifa ya Uefa, Eriksen aliwaambia waandishi wa habari: "Sitaki kukaa benchi kwa msimu msimu.

"Natumaini sio malengo ya kocha au klabu.

"Nina uhakika pengine nitapata dakika nyingi za kucheza na watu na natarajia mengi kwa wakati huu."



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# CAVANI AFUNGUKA KLABU KUMGOMBEA

Lakini aliamua kutua United kwa sababu ni moja ya klabu kubwa duniani na kwake...

**MANCHESTER,** England

EDINSON Cavani amedai alipata ofa nyingi kabla ya kukubali nafasi ya kujiunga na Klabu ya Manchester United.

**Straika huyo mwenye umri wa miaka 33, ambaye aliachwa na Paris Saint-Germain wakati mkataba wake ulipomalizika Juni mwaka huu, alikamilisha uhamisho wa kujiunga na United siku ya mwisho ya kufungwa kwa dirisha la usajili akiwa na kipengele cha kuongeza mwaka mmoja.**

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Uruguay alikuwa mmoja wa wachezaji waliohamia Old Trafford saa chache kabla ya dirisha kufungwa, baada ya United, ambao walichezea kichapo cha mabao 6-1 nyumbani kutoka kwa Tottenham, pia waliwasajili, Alex Telles, Facundo Pellistri na Adam Traore, ambao watawasili Januari.

Cavani alibainisa kwamba alifikiria kustaafu mwaka huu, lakini sasa yupo tayari kuanza maisha mapya ya soka kwenye Ligi Kuu England.

"Najihisi mwenye hamasa kubwa na kwa hakika nasubiria kwa hamu kuanza mazoezi na wachezaji wenzangu," alisema akiiambia tovuti ya klabu hiyo.

"Lakini kitu bora kuhusu klabu hii ni kwamba imeonyesha kuniamini kwa kunileta mimi.

"Kwa hakika nilitamani kuja hapa. Nina hamasa kubwa kujiunga na klabu hii kwa kabisa duniani.

"Nilikuwa na ofa nyingi mezani, (hata) wakati ambao mambo yalikuwa magumu kwa michezo yote duniani.

"Nilivutiwa sana na nafasi ya kucheza soka la Uingereza, na zaidi ni kwamba kujiunga na Manchester United, hicho kilikuwa kivutio kikubwa sana kwangu kwa sababu nilijiona bado nina nafasi ya kukamilisha kipindi changu cha kucheza.

"Ni nafasi yangu kuja hapa kwenye Ligi Kuu England, ligi ambayo inavutia sana, na ni moja ya ligi bora duniani kwa sasa. "Kwa upande wangu, hiyo ni heshima kubwa na nasubiria kwa hamu kuanza maisha kwenye changamoto mpya kwa kucheza kwenye Ligi Kuu England."

## ZISIKUPITE

### MESSI KUTUA CITY

MANCHESTER City watakuwa na nafasi kubwa ya kumsajili nyota wa Barcelona, Lionel Messi, mwenye umri wa miaka 33, kipindi kijacho cha majira ya joto kama nafasi hiyo ikitokea, Ofisa wa uendeshaji wa klabu hiyo, Omar Berrada amesema. ***(Manchester Evening News)***

### HAALAND SANCHO SOKONI

STRAIKA wa Borussia Dortmund na Norway, Erling Haaland mwenye umri wa miaka 20 na winga wa England, Jadon Sancho mwenye umri wa miaka 20, bado wapo kwenye orodha ya wanaowaniwa na Ole Gunnar Solskjaer pale Manchester United. ***(ESPN)***

### MADRID YAMKANA POGBA

REAL Madrid imeondoa uwezekano wa kumsajili kiungo wa Manchester United na Ufaransa, Paul Pogba mwenye umri wa miaka 27, baada ya kusema ana ndoto ya kuichezea klabu hiyo siku moja. ***(AS)***

### BRUYNE KUULA ZAIDI

KIUNGO wa Ubelgiji, Kevin de Bruyne mwenye umri wa miaka 29, anakaribia kusaini mkataba mpya ambao utamfanya alipwe mshahara wa pauni 300,000 kwa wiki pale Manchester City. ***(Sun)***

### SALIBA KUONDOKA ARSENAL

MLINZI wa Arsenal, William Saliba, raia wa Ufaransa mwenye thamani ya pauni milioni 27, bado hajaichezea klabu hiyo na sasa anatarajiwa kwenda kwa mkopo, huku klabu ya Ligi Daraja la Kwanza ya Brentford ikimwania nyota huyo mwenye umri wa miaka 19. ***(Goal)***

### WAARABU WAMTAKA MATA

KIUNGO wa Hispania, Juan Mata mwenye umri wa miaka 32, amepata ofa ili aondoke Manchester United kwenda kucheza soka la kulipwa nchini, Saudi Arabia. ***(Ian McGarry, via Mirror)***

### BALE DIMBANI SPURS

MSHAMBULIAJI wa Timu ya Taifa ya Wales, Gareth Bale mwenye umri wa miaka 31, anatarajia kuichezea mechi yake ya kwanza klabu yake ya Tottenham dhidi ya West Ham wikiendi ijayo.. ***(Telegraph)***

### GIROUD ALIKARIBIA ITALIA

FOWADI wa Chelsea na Ufaransa, Olivier Giroud mwenye umri wa miaka 34, amesema alikaribia kuhamia Ligi Kuu Italia, Serie A. ***(RMC Sport, via Football London)***

### GUARDIOLA KITAELEWEKA

MANCHESTER City wana matumaini, Pep Guardiola atasaini mkataba mpya wa kuendelea kuinoa klabu hiyo. ***(Telegraph)***

### WILSHERE AITAJA LALIGA

KIUNGO wa Uingereza, Jack Wilshere, 28, anataka kujiunga na klabu mojawapo inayoshiriki Ligi Kuu Hispania, La Liga, au Ligi Kuu Italia, Serie A. ***(Talksport)***

### ERIKSEN: NILIVURUGWA

KIUNGO wa Timu ya Taifa ya Denmark, Christian Eriksen (28), ambaye alikuwa akiichezea Tottenham amesikitishwa na hali ya kutokuwa na msimu mzuri iliyosababisha kukaa benchi ka muda mrefu kwenye kikosi cha Inter Milan. ***(Independent)***

# HABARI MICHEZO

## KMC yataja siri kuhamia Mwanza

**Na Mwandishi Wetu**

MABOSI wa KMC wamesema wametumia fursa ya kuitangaza timu yao kwa kuupeleka mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara kati yao dhidi ya Yanga utakaochezwa Oktoba 25, mwaka huu jijini, Mwanza ili kuongeza idadi ya mashabiki.

Awali mechi hiyo ilitarajiwa kufanyika kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini, Dar es Salaam lakini sasa mchezo huo utachezwa kwenye Uwanja wa CCM, Kirumba.

Ofisa Habari wa KMC, Christina Mwagala, alisema klabu yao imetumia nafasi iliyopitishwa na Bodi ya Ligi ya kuchagua uwanja huru ambao unaweza kutumika kwenye mechi mbili za msimu kwa kila timu.

"Katika kikao cha ufunguzi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, bodi ilieleza kuwa timu yeyote inaruhusiwa kucheza michezo yake miwili ya nyumbani nje ya kituo 'mama', hivyo sisi kama KMC FC tumetumia nafasi hiyo kuupeleka mchezo wetu jijini Mwanza," alisema Mwagala.

Mbali na hivyo, KMC pia inatambua thamani ya mashabiki waliopo katika mikoa mingine mbalimbali hapa nchini na kwamba malengo yao ni kutoa burudani kwa kila eneo hapa nchini.

"Tunafahamu tuna mashabiki wengi kwenye kila mkoa, hivyo ni nafasi kwa watu wa Mwanza kujitokeza kwa wingi siku hiyo ili kushuhudia soka safi linalochezwa na timu ya KMC FC, na hivyo itakuwa ni salamu tosha kwa timu nyingine kongwe kuona ubora wa kikosi chetu." aliongeza.

## Shein awafunda wanaopenda soka

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, amewaambia wadau wa soka kutumia kitabu kipya alichokizindua kiitwacho "Mwalimu Bora wa Soka" kama chuo kwa wachezaji wa mpira wa miguu pamoja na makocha wa mchezo huo walioko ndani na nje ya Zanzibar.

Dk. Shein aliyasema hayo juzi katika Ukumbi wa Sheikh Idrisa Abdulwakil, Kikwajuni, jijini Zanzibar, katika hafla ya uzinduzi wa kitabu hicho kilichoandikwa na Kocha, Gullam Abdallah Rashid na kuhudhuriwa na viongozi mbalimbali pamoja na wanamichezo.

Kiongozi huyo ambaye aliwahi kuwa mwanamichezo maarufu hapa Zanzibar miaka ya nyuma alisema kitabu huandikwa ili kisomwe, hivyo ana amini kitabu hicho kitawavutia idadi kubwa ya wasomaji ili malengo ya kuinua mpira wa miguu yatimie.

Alisema mwandishi wa kitabu hicho hakukiandika kwa kubahatisha, bali amekiandika kwa umahiri na weledi mkubwa kwa sababu yeye ni mwanasoka wa zamani. Alimtaja mtunzi wa kitabu hicho ambaye mbali na nafasi mbalimbali za uongozi, lakini amewahi kuichezea Timu ya Taifa ya Zanzibar (Zanzibar Heroes) pamoja na ile ya Bara (Taifa Stars).

Alisema naye amepata mafanikio katika maeneo mbalimbali kutokana na heshima na nidhamu kubwa aliyokuwa nayo.

# MABAO KIDUCHU, USHINDANI VYATAWALA 'DABI' YA MBEYA

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JIJI la Mbeya ni miongoni mwa mikoa michache yenye timu nyingi zinazoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara katika msimu wa 2020/2021, ambao unashirikisha jumla ya timu 18.

**Mbeya una timu tatu zinazoshiriki ligi hiyo ambazo ni pamoja na Tanzania Prisons, Mbeya City na wageni wa Ligi, Ihefu FC.**

Mbali na Mbeya kuwa na timu nyingi za ligi Kuu, pia ndio Mkoa wa pili kwa sasa kuwa na timu zenye ushindani wa muda mrefu maarufu kwa jina la 'Dabi' ikizihusisha Timu za 'Wagonga nyundo' Mbeya City na 'Wajelajela' Tanzania Prisons.

Ushindani wa Mbeya City na Tanzania Prisons ulianza msimu wa 2013/14, baada ya Mbeya City kupanda daraja ikiwa ni mwaka mmoja baada ya kaka zao kupanda ligi hiyo.

Mpaka sasa timu hizo zimekutana kwenye mechi za ligi kuu mara 15 na zimefungana mabao 21 pekee sawa na wastani wa bao 1.4 katika kila mchezo.

Kati ya mabao yaliyofungwa na timu hizo, Tanzania Prisons wanaoongoza kuzifumania nyavu za wapinzani wao kwa kufunga mabao 11 ambayo ni goli moja zaidi ya Mbeya City ambao wamefunga mabao 10.

Vilevile kati ya michezo hizo 15, Tanzania Prisons wamepata ushindi kwenye michezo mitano ikiwa ni mchezo mmoja zaidi ya City ambao wamepata ushindi kwenye michezo minne huku zikitoka sare kwenye michezo sita.

Kwenye michezo hiyo 15, mchezo uliokuwa na mabao mengi ni wa Januari 14, 2018 ambao ulikuwa mchezo wa mzunguko wa kwanza kwenye msimu wa 2018/2019 ambapo ulikuwa na mabao matano, Tanzania Prisons akiwa mwenyeji alipata ushindi wa mabao 3-2.

Michezo mingine iliyozikutanisha timu hizo ilikuwa na mabao kiduchu na mingine ilikuwa haina mabao kabisa kwa kila timu kulinda nyavu zake zisitikiswe na mpinzani wake.

Katika msimu wa 2013/2014 ambao ulikuwa wa kwanza kwa Mbeya City kushiriki Ligi Kuu, timu hiyo ikiwa katika kiwango bora ilipata ushindi kwenye michezo yote miwili, mzunguko wa kwanza wakiwa wenyeji walipata ushindi wa mabao 2-0 na katika mechi ya marudiano waliwachapa 'ndugu' zao bao 1-0 huku kwenye msimamo wa ligi City wakimaliza nafasi ya tatu.

Msimu uliofuata wa 2014/15 mambo yalibadilika ambapo kwenye mzunguko wa kwanza timu hizo zilitoka sare ya mabao 2-2 na mzunguko wa pili hali ikawa mbaya kwa Mbeya City ambapo iliambulia kipigo cha goli 1-0 huku Prisons ikishinda 1-0 na timu hizo kutoka suluhu mechi ya marudiani katika msimu uliofuata.

Msimu uliopita, ambapo Mbeya City iliponea kwenye tundu la sindano kushuka daraja, mzunguko wa kwanza timu hizo zilitoka suluhu na waliporudiana City walipata ushindi mwembamba wa 1-0.



Wachezaji wa Simba wakiwa katika mazoezi ya viungo kwa ajili ya kujiandaa na mechi ya raundi ya sita ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Tanzania Prisons, itakayochezwa Oktoba 22, mwaka huu. **PICHA: MTANDAO**

# Chirwa awaomba radhi Wazambia

**Na Saada Akida**

MSHAMBULIAJI wa Azam FC, Obrey Chirwa, amesema sababu ya kutojiunga na kikosi cha Timu ya Taifa ya Zambia (Chipolopolo) ni kuchelewa kupata cheti cha COVID 19 ambacho kilimfanya akose safari ya ndege.

Akizungumza na gazeti hili jijini, Dar es Salaam, Chirwa alisema alilazimika kupata kibali cha COVID 19 ili asafiri kwenda nchini nyingine, sheria ambayo imewekwa nchini kwao.

Chirwa alisema baada ya kutafakari juu ya kile kilichotokea kwa kushindwa kuungana katika kikosi cha timu hiyo, anaomba msamaha kwa benchi la ufundi, wachezaji wenzake pamoja na uongozi wa Zambia.

"Nimeshindwa kusafiri sababu nilikuwa na majukumu kwenye klabu yangu, tulicheza mechi Oktoba 4 na 5, mwaka huu, nikatakiwa kwenda Zambia, ili kujiunga na Timu ya Taifa, lakini nilichelewa kupata cheti hicho na kupoteza nafasi ya kusafiri," alisema Chirwa.

Alisema ndege waliyotumia haikuwa ya moja kwa moja, lakini anaelewa haikuwa uamuzi wake, kama mchezaji anahitaji kuonyesha mfano wa kuomba radhi wadau wa soka nchini Zambia.

"Nahitaji kuonyesha mfano wa kuigwa, naomba msamaha kwa wananchi wa Zambia na Chama Cha Soka (FAZ), kwa kutokwenda kutokana na sababu zilizopo nje ya uwezo wangu," alisema Chirwa.

Aliongeza anamshukuru kocha wake wa Zambia kwa kumwita kwenye kikosi chake na anaamini tatizo hilo halitajitokeza wakati mwingine.

Michezo
Jumapili Oktoba 11, 2020
Nipashe



Cavani afunguka klabu kumgombea UKURASA 22

# STARS, BURUNDI MECHI YA KISASI

## ●●● Majaliwa mgeni rasmi katika mchezo huo ambao...

**Na Somoe Ng'itu**

MUDA umefika! Baada ya tambo na majigambo ya hapa na pale, hatimaye mechi ya kirafiki ya kimataifa kati ya wenyeji, Tanzania (Taifa Stars), dhidi ya Burundi inatarajiwa kuchezwa leo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini, Dar es Salaam.

**Taifa Stars itashuka uwanjani ikiwa na kumbukumbu ya kuwaondoa Burundi kwa penalti 3-0 katika mechi za kuwania kuingia hatua ya makundi ya mashindano ya Kombe la Dunia. Matokeo ya jumla yalikuwa ni sare ya mabao 2-2.**

Stars inatumia mechi ya leo kujiandaa kuikabili Tunisia katika mchezo wa kwanza wa Kundi J utakaochezwa Novemba 13, mwaka huu jijini, Tunis na marudiano hapa nchini ifikapo Novemba 17, mwaka huu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Taifa Stars, Etienne Ndayiragije, alisema timu yake imefanya maandalizi mazuri kuelekea mchezo huo na anaamini watainga uwanjani kupambana kusaka matokeo mazuri.

Ndayiragije alisema mechi hiyo itakuwa na ushindani kwa sababu ya changamoto ya wachezaji wa makocha kufahamiana, hivyo wanahitaji kuongeza umakini na kutumia vizuri nafasi zitakazopatikana.

Kocha huyo wa zamani wa Azam FC, KMC na Mbao alisema kila mchezaji yuko tayari kwa mchezo huo ambao atamkosa mshambuliaji tegemeo, John Bocco, ambaye ni majeruhi.

"Vijana wako vizuri, wana hali nzuri, kile ambacho nilikihitaji kukiona, nimeona, kuona muunganiko na nimeuona baada ya mazoezi, tutarajie kupata matokeo mazuri, kila mmoja anahitaji kupata ushindi, tuombe Mungu kama mtihani wa Jumapili tunaufanya vizuri," Ndayiragije alisema.

Aliongeza kila mchezaji katika kikosi hicho ana umuhimu na mchango wa pamoja ndio utakaosaidia kupata matokeo chanya katika mechi hiyo.

Nahodha Msaidizi wa Taifa Stars, Aishi Manula, alisema wamejiandaa vizuri na wako tayari kwa mpambano huo kutokana na historia na rekodi ya timu hizo mbili.

"Tunaamini mechi itakuwa ngumu na yenye ushindani, mara nyingi tunapocheza na majirani huwa tunakutana na mchezo mgumu, ni mechi itakayotufanya tujue tuko katika nafasi gani, kuelekea michezo inayofuata, tutapigana jasho na damu ili kuonyesha kile tulichokuwa nacho," alisema Manula.

Aliwataka mashabiki na Watanzania kujitokeza kwa wingi kuishangilia ili kuipa timu hiyo hamasa. Naye Kocha Mkuu wa Burundi, Jimmy Ndayizeye, alisema kikosi chake kimejipanga kuelekea mchezo huo na

"Tunajua walitutoa katika mechi za kuwania tiketi ya makundi ya kushiriki Kombe la Dunia, hiyo ilishapita, sasa tumekuja kufanya kila kitachowezekana ili kupata ushindi," alisema kocha huyo.

Saido Berahinho, nahodha wa Burundi, alisema walisikitika kupoteza mchezo uliopita walipokutana na Tanzania, lakini sasa wana kikosi imara na chenye damu mpya kilichojipanga kupata ushindi.

Berahinho alisema wanahitaji kurekebisha makosa ya nyuma na hatimaye kupata ushindi kwenye mechi ya leo.

**MAJALIWA MGENI RASMI**

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi katika mchezo huo utakaofanyika kuanzia saa 10:00 jioni na kuchezeshwa na refa, Martin Saanya kutoka Morogoro.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Hassan Abbasi, alisema serikali inawahamasisha Watanzania kujitokeza uwanjani kwa wingi kuishangilia Taifa Stars ambayo inatumia mechi ya leo kujiandaa na michezo mingine ya kimashindano itakayoanza baadaye mwezi ujao.



Nahodha wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), Mbwana Samatta, akifanya mazoezi kujiandaa na mechi ya kirafiki ya kimataifa dhidi ya Burundi itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, jijini Dar es Salaam. Kushoto ni Thomas Ulimwengu na Jonas Mkude.
**PICHA: MTANDAO**

# Yanga yajenga timu ya dk 120

**Na Adam Fungamwango**

KAIMU Kocha Mkuu wa Yanga, Juma Mwambusi amesema anataka kuwaimarisha wachezaji wa timu hiyo waweze kucheza kwa spidi na kiwango kile kile bila kuchoka ndani ya dakika 90 hadi 120.

Mwambusi alisema hayo baada ya mechi ya kirafiki kati ya timu yake dhidi ya Mwadui FC iliyofanyika kwenye Uwanja wa Azam Complex na kushinda bao 1-0, juzi usiku.

Kocha huyo alisema mechi za kirafiki wanazocheza zinasaidia kuimarisha viwango vya wachezaji wake, hasa wale ambao hawachezi mara kwa mara, lakini pia kusahihisha makosa yanayojitokeza.

"Wachezaji wote ni wa Yanga, wamesajiliwa na wanatakiwa kucheza, hivyo wale ambao hawachezi ni wajibu wetu kuwaangalia nao, kuimarisha viwango vyao ili waisaidie timu,"alisema Mwambusi.

Aliongeza jambo lingine ni kwamba anataka kuona wachezaji wake wanacheza katika ubora wa juu kwa muda wote wa mchezo na hii ndiyo itawasaidia kupata ushindi bila tabu.

"Ninataka kuona wanakuwa na uwezo wa kucheza dakika zote 90 hadi 120 bila kuchoka, lakini kwa kiwango kile kile na spidi ile ile. Nadhani baada ya wiki tatu hivi vyote tunavyovifanyia kazi vitaanza kuonekana na kutoa matokeo mazuri zaidi," alisema Mwambusi.

Kuhusu mchezaji raia wa Angola, Carlos Carlinhos, kocha huyo alisema kuwa bado hajapata utimamu wa mwili wa kutosha, hivyo wana kazi ya kumjenga fiziki ili aweze kufanya kile ambacho watamtuma.

"Bado anatakiwa apate fiziki ya kutosha na akishakuwa vizuri tunaweza kupata kile ambacho tunatarajia zaidi kutoka kwake, zaidi ya faulo na kona," Mwambusi alisema.

Mwambusi anaiongoza Yanga baada ya mabosi wao kumtimua, Zlatko Krmpotic huku Mrundi, Cedric Kaze, akitarajiwa kuwasili nchini wakati wowote kuchukua mikoba ya Mserbia huyo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >